

KUCHUNGUZA ITIKADI KATIKA MASHAIRI YA MUHAMMED SEIF

KHATIB: MIFANO KUTOKA DIWANI YA WASAKATONGE

MEIJO LOLOINYO LAIZER

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI
KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2023

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibithisha kuwa ameisoma tasnifu hii inayohusu ‘*Kuchunguza Itikadi katika Mashairi ya Muhammed Seif Khatib: Mifano kutoka Diwani ya Wasakatonge*’ na ameridhika kwamba kazi hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inastahili kuwasilishwa kwa ajili ya Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

Tarehe.....

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwa kuiga wala kunakili kwa namna yoyote ili tasnifu hii, kwa njia ya kieletroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vinginevyo bila ya kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi **Meijo Loloinyo Laizer**, nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunikiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili au shahada nyingine yoyote.

.....
Sahihi

.....
Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa Wazazi wangu Wapendwa pamoja na familia yangu yote. Pia ninaitabaruku kazi hii kwa wananchi wote wa Wilaya ya Siha.

SHUKURANI

Awali ya yote shukurani zangu dhati kabisa natoa kwa Mwenyenzi Mungu kwa kunipa nguvu na afya njema muda wote na kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Vilevile, natoa shukurani kwa rafiki zangu wote walionitia moyo wakati wote wamasomo kwani wamekua msaada mkubwa katika kutimiza ndoto zangu za kupata elimu ya juu katika shahada ya uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na sasa nimehitimu. Pia, sina budi kutumia fursa hii kumshukuru sana msimamizi wangu wa tasnifu hii, Dkt. Mohammed Omary Maguo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya kazi hii. Hakusita wala kuchoka katika kunishauri na kunirekebisha katika kazi hii kwa hatua zote mpaka ilipokamilika. Usaidizi wake haupimiki wala kulipika. Ninachoweza kusema kwako Mwalimu wangu Dkt. Mohammed Omary Maguo, nasema tena Ahsante sana na Mwenyenzi Mungu akupe afya njema na maisha marefu kwa manufa ya jamii zima.

Halikadhalika shukurani zangu ni kwa wanafunzi wenzangu wa Shahada ya Uzamili Kiswahili katika Idara ya Lughu na Taaluma za fasihi kwa ushirikiano wao walionipatia katika muda wote wa masomo yangu na kunitia moyo pale nilipofikia kukata taama na kunipa mawazo pale nilipokwama katika tasnifu yangu.

Pia, natoa shukurani zangu kwa familia yangu na kwa mke wangu kipenzi Suzana Oyoho na Watoto wangu Saruni Meijo, Melita Meijo na Saitoti Meijo kwa uvumilivu wao mkubwa alionesha katika kipindi chote cha masomo kutohana na kunikosa nyumbani kwa muda mrefu na kwa kunisaidia kunitia moyo pale nilipofikia hatua ya kukata tamaa ya kuendelea na tasnifu hii.

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kabisa, kwa Wahadhiri wangu wote waliofundisha na kushauri katika hatua zote za kozi hii ya Shahada ya Uzamili ambao ni Profesa Emanuel Mbogo, Dkt. Zelda Elisifa na Dkt. Peter Lipembe. Hakika mchangao wao ni mkubwa sana kwani umeweza kunisaidia kupata ujuzi na maarifa mapya katika nyanja mbalimbali katika kazi ya fasihi na hatimaye sasa kukamilisha kazi hii kwa ufanisi mkubwa sana.

Vile vile, namshukuru sana Dkt. Tatu Mhadhiri kutoka chuo kikuu cha Dodoma kwa kuweza kunisaidia muda wote wa utafiti na kunipatia ushauri wa mara kwa mara kwa hatua zote za kazi yangu, hakika siwezi kumlipa ila Mwenyezi Mungu aweze kumbariki.

Mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Afisa Elimu wangu wa Halmashauri ya wilaya ya Arusha Bw. Menard Lupenza na Afisa Elimu Halmashauri ya Wilaya ya Hanang Bi. Elizabeth Lussingu na wafanyakazi wenzangu wa Idara ya Elimu Sekondari halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kwa kunishauri na kunitia moyo katika kipindi chote cha masomo yangu.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza itikadi katika mashairi ya Muhammed Seif Khatib katika Diwani ya Wasakatonge. Katika kukamilisha tasnifu hii, utafiti ulikuwa na malengo mahususi mawili ambayo ni kuchambua masuala ya kiitikadi yanazojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge* na kubainisha mbinu za kisanaa zinazoibua masuala ya kiitikadi katika mashairi ya *Wasakatonge*. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka kwa kuongozwa na nadharia mbili za U-marx na Simiotiki. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba masuala yanayojenga itikadi katika mashairi ya *Wasakatonge* ni, uongozi mbaya, uchu wa madaraka na uongozi, mapenzi, matabaka, ukoloni mamboleo, malezi na maadili katika jamii. Pia matokeo ya utafiti huu, yanaonyesha kuwa itikadi katika mashairi ya *Wasakatonge* zinajengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kama tamathali za usemi za tashibiha, sitiari, takriri na misemo tu ndizo zilizotafitiwa. Kupitia vipengele hivyo vya fani, mtunzi ameweza kuwasilisha itikadi mbalimbali katika kazi yake ya fasihi kwa Mashairi ya *Wasakatonge*.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI.....	iii
TAMKO	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI..	viii
YALIYOMO.....	ix
VIFUPISHO.....	xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	6
1.4 Lengo Kuu la Utafiti.....	6
1.4.1 Malengo Mahususi	7
1.5 Maswali ya Utafiti	7
1.6 Umuhimu wa Utafiti	7
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	8
1.8 Mpangilio wa Tasnifu.....	8

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA

KINADHARIA 9

2.1 Utangulizi	9
2.2 Mapitio kuhusu Ushairi wa Kiswahili.....	9

2.3	Mapitio Kuhusu Mashairi ya Mohammed Seif Khatibu	12
2.4	Suala la Itikadi kwa Ujumla	13
2.5	Itikadi katika Fasihi kwa Ujumla	14
2.6	Pengo la Maarifa.....	16
2.7	Mkabala wa Kinadharia.....	16
2.7.1	Nadharia ya U-Marx.....	16
2.7.2	Nadharia ya Simiotiki.....	19
2.8	Hitimisho	23
	SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	24
3.1	Utangulizi	24
3.2	Usanifu Utafiti	24
3.3	Eneo la Utafiti.....	25
3.4	Sampuli na Usampilishaji.....	25
3.4.1	Sampuli.....	25
3.4.2	Usampilishaji	26
3.5	Data za Utafiti.....	26
3.6	Mbinu za Kukusanya Data na Taarifa za Upili	27
3.6.1	Mbinu ya Usomaji Makini.....	27
3.6.2	Upitiaji Nyaraka	27
3.7	Uchambuzi wa Data	28
3.7.1	Mkabala wa Kimaelezo	28
3.8	Usahihi wa Data	28
3.9	Maadili ya Utafiti	29

3.10	Hitimisho	29
------	-----------------	----

SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA

DATA ZA UTAFITI..... 30

4.1	Utangulizi	30
4.2	Historia ya Mshairi Mteule Mohammed Seif Khatib	30
4.3	Itikadi katika Diwani Teule	31
4.3.1	Itikadi Zinazojitokeza katika Diwani ya <i>Wasakatonge</i>	31
4.3.2	Itikadi ya Kupiga Vita Uongozi Mbaya	32
4.3.3	Itikadi ya Demokrasia ya Kweli na Utu	34
4.3.4	Itikadi ya Ukoloni Mamboleo	36
4.3.5	Itikadi ya Matabaka katika Jamii.....	38
4.3.6	Itikadi ya Mapenzi	41
4.3.7	Itikadi ya Kufanya Kazi kwa Bidii.....	43
4.3.8	Itikadi ya Maadili na Malezi.....	44
4.2.9	Itikadi ya Uchu wa Madaraka na Uongozi	46
4.3.10	Itikadi ya Unafiki na Usaliti katika Jamii.....	47
4.2.10	Itikadi ya Dini	48
4.3.11	Itikadi ya Kimapinduzi	50
4.3.12	Itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea	51
4.4	Mbinu za Kisanaa katika Mashairi ya Wasakatonge.....	53
4.4.1	Sitiari	53
4.4.2	Tashibiha	54
4.4.3	Takriri	55

4.4.4	Ishara	57
4.4.5	Picha na Taswira.....	57
4.5	Hitimisho	58
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO		60
5.1	Utangulizi	60
5.2	Muhtasari.....	60
5.3	Hitimisho	62
5.4	Mapendekezo ya Utafiti	63
5.4.1	Mapendekezo kwa Wahakiki	63
5.4.2	Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari	64
5.4.3	Mapendekezo kwa Watunga Mitaala	64
5.4.4	Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye	65
5.4.5	Mapendekezo kwa Jamii	65
MAREJELEO:		67
VIAMBATANISHO		73

VIFUPISHO

B.A Ed Bachelor of Arts with Education

Dkt Daktari

EALB East Africa literature Bureau

EAP East Africa Press

M.A Masters of Arts

OUP Oxford University Press

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sura hii inajadili kuhusu tatizo lililoshughulikiwa katika utafiti huu kupitia vipengele vya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu. Kimsingi, sura hii imebainisha ni jambo gani ambalo limeshughulikiwa katika tasnifu hii.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Itikadi ni dhana inayorejelea maadili, imani, tabia, au mtazamo wa msanii kuhusu suala moja ama zaidi katika jamii. Itikadi inaweza kuwa ya mtu mmoja mmoja ama kikundi cha watu ama jamii fulani. Kwa mfano nchi ya Tanzania ilijulikana kwa kufuata msingi ya itikadi ya siasa ya ujamaa na kujitegemea hata baaada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha la mwaka 1967 (Mpangala, 1977). Kwa ujumla itikadi huongoza jamii na kuifanya jamii hiyo na watu wake wawe wafuasi wa imani ya itikadi ambayo ndio inayoongoza jamii hiyo (Shemweta, 2015).

Kwa msingi huo ni dhahiri kuwa, itikadi ni dhana inayorejelea imani, maadili, mtizamo, tabia pamoja na namna ama jinsi ya kufikiri na kuyaelewa mambo mbalimbali sawasawa na kaida za jamii ambazo huongoza katika namna ya kuamua na kukubali jambo mahsus. Itikadi ni moja ya kipengele cha maudhui katika kazi ya fasihi hivyo huonyesha mwelekeo na imani ya mwandishi kuhusu kile anachokiamini katika jamii yake. Namna anavyoyatazama mazingira yake, jinsi na mbinu za kuyatawala na kuyakabili mazingira hayo. Pia itikadi ni kipengele katika kazi za

fasihi na ni kipengele ambacho hubeba imani na mtazamo wa mwandishi kuhusu suala analolizungumzia katika jamii yake.

Kipengele cha itikadi bado hakijafanyiwa utafiti sana na watafiti wa mashairi ya Kiswahili hususani mashairi ya Mohhamed Seif Khatib. Haya tumeyabaini baada ya kupitia maandiko na kutalii kazi tangulizi na kuona bado itikadi katika mashairi ya Mohemmed Seif Khatib haijafanyiwa utafiti. Tulibaini kwamba wapo watafiti ambao wamejikita katika kuchunguza matumizi ya lugha yanavyouibia dhamira za kisiasa na matumizi ya picha na taswira katika mashairi ya mtunzi huyu (Pella, 2018).

Mulokozi na Kahigi (1982) wamesema ushairi ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum na fasaha, wenyewe muwala, kwa lugha ya picha, sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo Hali hivyo, huoneshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa ufupi ili kuonesha ukweli fulani wa maisha. Kwa mantiki hiyo, ushairi huwa ni chombo muhimu cha utamaduni wa jamii, kwa kuburudisha, huhifadhi historia, kujikomboa kutoka kwa madhalimu, kusifu, kukosoa, kukashifu na kushutumu maoni yasiyofaa. Kwa msingi huo, ushairi umetokana na jamii ya wanadamu wenyewe na umesheheni ukwasi mkubwa wa lugha ambayo imekuwa ukitumika katika hatua zote za kiitikadi katika Nyanja ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni (Mayoka, 1993).

Kihistoria, ushairi umetumika katika vipindi vyote ambavyo mwanadamu amepitia. Kwa mfano, tangu enzi za kuishi mapangoni, enzi za uwindaji, ujima, utumwa, vita vya makabila, uvamizi wa wageni, ukoloni na harakati za kupambana na ukoloni

hadi kupata uhuru (Mayoka, 1993). Hivyo, ushairi wa Kiswahili ni sanaa kongwe inayopiga hatua ya maendeleo siku hadi siku kutoka na maendeleo ya mwanadamu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Mabadiliko katika hatua hizi, yanaufanya ushairi wa Kiswahili nao kubadilika ili kuweza kuyasawiri maisha kama yalivyo. Mabadiliko hayo, yanaathiri hadi utunzi wa mashari. Hivyo, waandishi wanatunga mashairi ya kisasa ambayo ndiyo hasa yanayoendana na maisha ya sasa ya jami. Jamii ya sasa ni mchafu koge ambapo kila kitu katika jamii kinafanywa kwa vurugu vurugu tu na hakuna utaratibu wowote (Wamitila, 2008). Kwa mfano, katika jamii, kuna mtu mzima anambaka mtoto mdogo ambaye hajafikisha hata mwaka mmoja. Rushwa na ufisadi unatendeka kwa kiasi iliyokithiri. Wizi na ujambazi, uchawi pamoja na fitina kushamiri. Mambo haya yote yanahitaji aina ya ushairi ambao itaweza kusawiri kama yanavyojitokeza. Aina hiyo ya ushairi si nyingine bali ni ile isiyofuata kanuni zilizowekwa ama zilizo kuwao awali. Kwa muktadha huo, utagundua kuwa, ushairi wa Kiswahili imeweza kupita katika wakati mwingine kutohana na utunzi mkubwa wa mashairi ya kiti.

Katika karne ya ishirini, maendeleo ya ushairi wa kiswahili yaliathiriwa na mambo matatu ambayo ni elimu ya kizungu, hati ya maandishi ya Kirumi, na kuanzishwa kwa maktaba ya uchapaji wa vitabu na magazeti. Elimu ya kizungu ilielezea lugha ya Kiswahili katika maeneo bora kupitia shulen, maarifa ya kusoma na kuandikwa na maarifa ya arudhi (kanuni za utunzi). Hati ya maandishi ya Kirumi ilienea kupitia elimu, pia kupitia makanisani, na ilianza kutumiwa na watunzi badala ya hati ya Kiarabu. Hivyo, ushairi ulianza kusomwa na watu wengi zaidi hata wasiokuwa Waislamu, na baadhi yao walianza kutunga kama vile Mathias Mnyampala. Maktaba

yalisaidia kueneza utamaduni wa kusoma. Hivyo, magazeti mengi yaliyochapishwa kwa lugha ya Kiswahili na kusambazwa. Baadhi ya magazeti hayo yalikuwa na kurasa za mashairi ambazo zilisaidia kuwakutanisha watunzi kutoka sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki. Mfano mzuri ni gazeti la “*Mambo leo*”. Watunzi kama Mwinyi Hatibu Mohamed, Mahmoud Jitukali, Snow White na Hamis Amani Nyamaume walipata umaarufu wao kupitia gazeti hilo. Uchapishaji wa vitabu ulipoanzishwa ulisaidia kuikuza na kuieneza sanaa ya ushairi, hasa baada ya Shirika la uchapishaji vitabu la Afrika Mashariki (EALB) kuanzishwa. Baadhi ya watunzi mashuhuri wa miaka hiyo waliochapishiwa diwani zao na shirika hilo ni: Amri Abeid, Akili Mali Mnyampala na Sheikh Lambert.

Hivyo, ushairi umetumika katika vipindi mbalimbali vya maisha ya mwanadamu katika harakati za kupigania uhuru na baadae katika ujenzi wa jamii mpya kwa kujikombaa kiitikadi katika Nyanja za kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kiuchumi.

Baada ya uhuru, ushairi ulisambaa zaidi kutokana na msukumo wa kiitikadi za kisiasa na fani mpya kama vile: ngonjera na mavue (mtiririko au tungo -huru) vilianzishwa ili kuzingatia mahitaji mapya ya kisiasa na kisanii. Hii ikasaidia kubainisha ubunifu wa namna mfumo wa kisiasa katika mataifa ya Afrika Mashariki ulivyokuwa umejengwa katika muktadha wa udhalimu na udikteta katika harakati za kupigania uhuru. Baadhi ya viongozi walipaza sauti zao kuwa wao ni wateteaji wa maslahi ya wananchi na kupitia kwa matamko hayo waliaminiwa na kupewa majukumu hayo katika mataifa husika. Kwa mazingira hayo, ujumbe ukawasilishwa katika fani mbalimbali za fasihi, zilizozingatia miktadha halisi ya kijamii yalioibua ubunifu huo (Maitaria, 2012 na Nowottry, 1972).

Mwanzoni mwa miaka ya 1960 hadi kufikia 1990 mataifa ya Afrika Mashariki yakawa hayajathibithisha mfumo mwafaka wa kisiasa (Mpangala, 2004). Hii ni kutokana na mabadiliko ya ya kiitikadi kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyoibua mitazamo mbalimbali katika kukabiliana na dosari zinazolemaza masuala ya kisiasa, zinazoendelezwa katika utawala wa mataifa ya Afrika Mashariki. Katika miaka ya 2000, baadhi ya watu katika mataifa haya wamekuwa hawatosheki kuwa halaiki ya kutazama jinsi masuala ya siasa yanavyoburutwa na baadhi ya wale waliovishwa majoho ya uongozi. Kwa hiyo, ushairi wa Kiswahili ukatumwiwa kama zao la jamii na mawazo yanayowasilishwa huweza kutathiminiwa na kufasiriwa katika muktadha ya kimaeneo, kihistoria na kiwakati. Baadaye, watu hao walijawa kiburi kilichoelekezwa zaidi kwenye tamaa ya kujilimbikizia mali na wale waliomkweza walisahaulika. Mfano katika shairi la “Mnazi” katika *Sauti ya Dhiki* (uk.17-22) inabainishwa taswira hiyo ya kiongozi mwenye uchu wa kutaka kuendelea kushikilia uongozi na jitihada zake zipo katika kuipora rasilimali ya jamii kulingana na mshairi. Mwelekeo huo hauvumiliwi katika demokrasia iliyouhamasisha umma kujitolea kwa hiari kuupania na kuung’ang’ania ukombozi wanchi yao kutoka kwa utawala wa mkoloni.

Kimsingi katika uhalisia huu, ushairi wa Kiswahili umekuwa ukibainisha, kwa kuchochea tafakari katika bongo za watu, ili kuweza kuchukua hatua ya kushiriki kikamilifu katika harakati za masuala muhimu ya kitaifa kwa kuzingatia itikadi, siasa na uongozi stahiki kwa lengo la kufikia ujenzi wa jamii mpya katika jamii husika. Hali iliyosababisha kuibua watanzi anuwai ambao wameweza kubainisha vipengele mahususi katika kushughulikia dhamira za kijamii na kisiasa kwa udhati wake katika

jamii zao. Baadhi ya wasanii hao ni kama Mohammed Seif Khatibu, David Massamba, Euphrase Kezilahabi, na wengine wengi. Ni dhairi mpaka kufikia sasa hakuna utafiti wa kina ambao tayari umefanywa kuhusiana na “*Masuala ya kiitikadi kama msingi wa ujenzi wa jamii mpya kama inavyojitokeza katika mashairi ya Wasakatonge ya Mohammed S. Khatib*”. Utafiti huu umefanywa ili kuweza kuziba pengo hili la maarifa.

1.3 Tatizo la Utafiti

Ushairi wa Kiswahili ni fani pana ambayo imetafitiwa na wataalam mbalimbali kwa malengo na nia tofauti tofauti. Wapo watafiti ambao wamechunguza matumizi ya picha na taswira katika mashairi ya Mohamed Seif Khatib, Pella (2016), na wengine wamechunguza dhamira za kisiasa katika mashairi andishi kama Omary (2011), Habwe (1991), Folova (2003), Omari (2009), Msuya na Lukopela (2012). Ni dhahiri kuwa, waandishi hawa wameweza kufanya tafiti zao kwa lengo kutathimini namna watunzi wanavyoweza kujenga dhamira mbalimbali za kisiasa kwa kutumia lugha, picha na twasira katika kufikia ujenzi wa jamii mpya. Hata hivyo, mashairi ya Mohammed Seif Khatib hasa diwani *Wasakatonge* bado haijachunguzwa kwa kina katika kipengele cha itikadi. Baada ya kugundua jambo hili, ndipo sasa tukaamua kufanya utafiti huu ili kuziba pengo hilo la kiutafiti.

1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza suala la Itikadi katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib kupitia Diwani ya *Wasakatonge* pamoja na mbinu za kisanaa.

1.4.1 Malengo Mahususi

Utafiti huu una jumla ya malengo mahususi ambayo yatatimizwa:

- i. Kuchambua masuala ya kiitikadi yanayojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge*
- ii. Kubainisha mbinu za kisanaa zinazoibua masuala ya kiitikadi katika mashairi ya *Wasakatonge*.

1.5 Maswali ya Utafiti

- i) Ni masuala gani za kiitikadi yanayojitokeza katika mashairi za Mohammed Seif Khatib katika Diwani ya *Wasakatonge*?
- ii) Ni mbinu zipi za kisanaa zinazotumika na Mohammed Seif Khatib katika kujenga masuala ya kiitikadi katika Diwani ya *Wasakatonge*?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika taaluma ya fasihi, kitaaluma, kinadharia, kisiasa, kiutamaduni, kisera na kijamii. Kitaaluma, matokeo ya utafiti huu yatatoa mchango mkubwa katika kuongeza marejeleo katika fasihi ya Kiswahili hususani ushairi wa Kiswahili. Kinadharia, utatoa uthibitisho na umuhimu kwamba, nadharia za uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaaluma. Hivyo, watafiti wa baadaye wataona umuhimu wa kutumia nadharia ya Ki-marx na nadharia ya Simiotiki katika uchambuzi wa kazi za fasihi. Hivyo, kwa upande wa wanafunzi wanaosoma shahada za awali, uzamili na uzamivu; tasinifu hii itatoa dira na mwongozo katika chambuzi za kazi za fasihi hasa katika uwanja wa fasihi watatumia utafiti huu kama sehemu ya marejeleo ya kuwasaidia kupata tatizo la utafiti na kuimarisha maandiko ya kazi

tangulizi katika tafiti zao. Utafiti huu utatoa mchango katika kuelewa itikadi ya Mohammed Seif Khatib kuhusu masuala ya kijamii katika muktadha wa jamii yake. Kupitia kazi za fasihi, utafiti huu utatoa mchango wa maarifa katika fasihi ya Kiswahili hususani mashairi ya Kiswahili.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza masuala ya kiitikadi katika diwani ya *Wasakatonge* ilioandikwa na Mohammed Seif Khatib. Diwani hii imeteuliwa kwa sababu ndio hasa inajibu maswali ya msingi katika utafiti wetu kwa namna ilivyokusudiwa. Utafiti umeongozwa na nadharia ya Ki-marx na nadharia ya Simiotiki na kuchambuliwa kimaelezo. Tasinifu hii imechambua itikadi pamoja na mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi wa *Wasakatonge* katika kuibua masuala ya kiitikadi.

1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii ina jumla ya sura kuu tano ambapo sura ya kwanza ni utangulizi ambao umewasilisha vipengele vya usuli, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za kukusanya na kuchambua data pamoja na vipengele vyote saidizi katika kukusanya data za utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na sura ya nne ni hitimisho, muhtasari na mapendekazo.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa kuzamia maandishi ya nyuma ambayo hufananishwa na taarifa hai zilizopatikana ndani ya utafiti wa sasa (Enon, 1998). Hivyo, humpa mtafiti msingi wa kinadharia, kanuni za utafiti wake kwa kuangalia nadharia alizotumia na watafiti walio tangulia (Orodho, 2005; Kombo na Tromp, 2011 na Bryan, 2012). Hivyo basi, katika sura hii tumepitia na kujadili kazi tangulizi kuhusiana na mada yetu ya utafiti ilikuweza kuona watafiti waliotangulia wanazungumza nini kuhusiana na mada tulioikusudia katika utafiti huu ili kubainisha pengo la kiutafiti lililoachwa na watafiti watangulizi.

Sura hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo; sehemu ya kwanza inahuu dhana ya ushairi, sehemu ya pili ni tafiti kuhusu kazi za ushairi, historia fupi ya mashairi, dhamira na fani katika kazi za fasihi na kuangalia nadharia zilizoongoza utafiti huu.

2.2 Mapitio kuhusu Ushairi wa Kiswahili

Senkoro (1968) anaelezea mwamko wa kisiasa katika mashairi ya Shaaban Robert. Anasema kwamba, nguli huyu wa fasihi ya Kiswahili, alikuwa ni mtaalamu wa kutumia lugha na mandhari ya kuhamasisha umma kudai haki zao bila ya mdaiwa kutambua hilo kwa haraka. Suala hili linaonekana katika *Insha na Mashairi* anavyowasilisha dhamira hiyo kwa kutumia luhga ya kisiasa.

Sanka (1994) anasema kwamba, ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuhifadhi historia, falsafa na utamaduni wa jamii. Hivyo, ni zao la jamii husika na huwa na sifa maalumu kulingana na muktadha lengwa na kwa jamii hiyo. Mawazo haya ya Sanka

(khj) yatasaidia kufikia malengo mahususi katika utafiti wetu kwani wametuwezesha kujua kuwa ushairi ni chombo muhimu katika kusawiri, kuononesha, kuelezea jambo fulani, wazo, au tukio, kuhifadhi historia, falsafa na utamaduni katika jamii; kulingana na muktadha lengwa kwa kuchambua masuala ya kiitikadi. Hivyo basi, kutokana na mawazo hayo tumewezesha kuchunguza masuala ya kiitikadi katika diwani ya *Wasakatonge*.

Frolova (2003) anasema kwamba, Kezilahabi hazungumzii siasa katika mashairi yake ya *Karibu Ndani*, (1988) bali anazungumzia masuala ya watu binafsi. Omary (2011) anamjibu Frolova kwa kusema kuwa, kezilahabi ni bingwa wa kuelezea masuala ya kisiasa katika mashairi yake yasiyofuata urari wa vina na mizani. Anatoa mifano ya matumizi ya lugha kisitiari, mafumbo na ishara ndiyo yanayoibua masuala ya kisiasa katika mashairi ya Kezilahabi. Japo katika utafiti wetu hatuzungumzii masula ya siasa mawazo haya yana umuhimu kwa kuwa yametusaidia kuona namna masuala ya kiitikadi yanavyojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge*.

Naye, Ismail (2012) anasema kuwa, mashairi hutumika kwa kiasi kikubwa kama chombo cha kuelimisha jamii kuhusiana na haki za binadamu, anaendelea kusema kuwa, muziki wa bongo fleva umekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za binadamu kutokana na madhila yanayomkabili binadamu. Ingawa kwa kiasi kikubwa habainishi kitu gani kifanyike ili kuondokana na madhila haya, ukweli ni kwamba muziki wa bongo fleva unaonesha jamii ilivyo na inakoelekea. Hivyo, mawazo haya yamesaidia kuononesha jinsi masuala ya kiitikadi yanavyojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge* ambayo Ismail (khj) hakuyazungumzia.

Alhabib (2012) anasema kuwa, wasanii wa nyimbo za taarab hutumia tawira mbalimbali kuchora na kuwasilisha masuala ya kisiasa katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni rushwa, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi, udini, ukabila, njaa, maradhi na ujinga. Kwa maelezo yake, mambo haya ni adui mkubwa katika kufikia ujenzi wa jamii mpya. Andiko hili limetusaidia katika utafiti wetu kwa kutuongoza katika kuchunguza masuala ya kiiikadi yanayojitokeza katika *Wasakatonge*.

Hassan (2018) amezungumzia masula ya ujaala katika ushairi wa Kiswahili. Katika andiko lake, ameelezea muktadha wa kisiasa kuwa ni mióngoni mwa miktadha inayoibua ujaala huo. Kimsingi, Hassan alipozungumzia masuala ya ujaala, ametoa mwanga kwa mtarufi ya kuona kuwa masuala ya kisiasa ni itikadi kwani yana mchango katika kuibua masuala muhimu kama vile ujaala. Hivyo, andiko hili limesaidia kubaini masuala ya kiiikadi yanayojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge*. Pia tumebaini kwamba, itikadi ndio huamua hatima ya nyanja nyingine za maisha; yaani, ni vigumu kutenganisha itikadi na mfumo mzima wa maisha ya jamii na hii imesaidia kusukuma mbele utafiti wetu.

Abdulla (2019) amezungumzia vitushi katika ushairi wa Kiswahili. Anaeleza matukio yanayoibua vitushi hivyo kuwa ni pamoja na matukio ya kisiasa kama vile rushwa na uongozi mbaya. Ingawa Abdulla (khj) hakuzungumzia masuala ya kiiikadi, kazi yake imempa mwanga mtarufi wa kuona kuwa ipo haja ya kuchunguza masuala ya kiiikadi katika mashairi ya *Wasakatonge* kwa sababu ye yé hakuyazungumzia.

2.3 Mapitio Kuhusu Mashairi ya Mohammed Seif Khatibu

Alhabib (2022) anasema kuwa, mashairi ya Muhammed Seif Khatibu yanaelezea masuala ya wavuja jasho yanaomulika uozo wa jamii. Hivyo, yanazindua umma kuhusu masuala ya wanasiasa wanaotumia nguvu za dola kwa maslahi yao binafsi. Andiko hili limemfanya mtafiti kuvutiwa kuchunguza masuala ya kiitikadi yanayojitokeza katika *Wasakatonge* ili kubainisha itikadi zinazofungama na masuala ya wavuja jasho.

Mrekwa (2013) amegusia kipengele cha maudhui katika diwani za *Wasakatonge* na *Fungate ya uhuru*. Mtaalam huyu anamtaja Muhammed Seif Khatib kuwa ni mtunzi aliyejitokeza na kuandikia mambo yanayohusu jamii na mabadiliko yake. Mambo hayo ni pamoja na uongozi mzuri, uongozi mbaya, demokrasia, rushwa, ufusadi, ukatili wa kijinsia, udikteta na usawa wa kijinsia. Kwa hakika mambo haya ndimo ndani yake mna mnawenza kuibuliwa itikadi na sisi tumeyazingatia katika utafiti wetu.

Mtandao (2017) anasema kuwa, kundi kubwa la mashairi ya *Fungate ya Uhuru* ni ya kisiasa. Mashairi hayo yana dhamira kama vile haki, wizi, rushwa uongozi mbaya, mnyonyaji, ufujaji wa mali, ukasuku na uzalendo. Dhamira hizi zimemuongoza mtafiti katika kuchambua masuala ya kiitikadi katika *Wasakatonge* kwa sababu yumkini na humo zitajitokeza kama ilivyo katika *Fungate ya Uhuru* maana yote ni mashairi ya Muhammed Seif Khatibu.

Pella (2018) amefanya utafiti na kuchambua mashairi ya mohammed Seif Khatibu kwa kuchunguza matumizi ya lugha katika kuibua dhamira za kisiasa na mwingine kuchunguza picha na twasira zinazojitokeza katika mashairi. Kimsingi, ndani ya

dhamira za kisiasa ni rahisi kuiona itikadi ya mwandishi ikijitokeza. Dhamira hizo za kisiasa zimetusaidia kuziona itikadi na kuifanya kazi yetu kuwa na uhakika kwamba uchunguzi wa itikadi katika Wasakatonge utafanikiwa. Hivyo basi kutokana na tafiti hizi tumepata mwanya wa kupata pengo la utafiti kwa kushughulika na itikadi katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib kama tulivyokusudia.

2.4 Suala la Itikadi kwa Ujumla

Itikadi ni dhana ambayo imeelezwa na wataalamu mbalimbali kutokana na ukweli kuwa kila jamii inaongozwa na itikadi fulani katika kufanikisha maisha yake ya kila siku. Adorno na Wenzake (1950) wanasema kuwa itiikadi ni maoni na mwenendo wa kufikiri juu ya maisha ya mwanadamu na jamii yake katika vipengele vya siasa, uchumi, dini, utamaduni na masuala ya kijamii kwa ujumla. Hivyo basi, itikadi waliyonayo wanajamii kuhusu maisha ndiyo itakayowaongoza katika kufikiri na kutafakari kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao kwa maana ya kufanikiwa au kutofanikiwa. Mawazo haya yanaungwa mkono na Loewenstein (1953) kwa kusema kuwa, itikadi ni imani na tafakuri inayoeleza mtazamo wa mwanadamu kuhusu mfumo mzima wa maisha yake.

Kwa mujibu wa Shemweta (2015) katika utafiti wake akimnukuu, Mcclocky (1964) anasema kwamba, itikadi ni mfumo wa imani ambao unaeleza, kujumuisha na kufafanua masuala ya madaraka, haki za binadamu na kutathimini masuala ya kihistoria ili kufanya maamuzi sahihi kwa wakati uliopo na ujao. Hapa ni dhairi kabisa kuwa Itikadi ndio msingi halisi inayoeleza namna ya kuwapata viongozi katika jamii na ni aina gani ya viongozi wanaohitajika katika jamii husika. Sambamba na hilo Itikadi ndiyo inayobainisha na kutoa mwongozo wa haki za

kibinadamu katika jamii husika kwa kusema haki husika na haki hizo zitawafikia vipi watu wanaostahiki kuzipata. Itikadi ni mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo wa kiuchumi au kisiasa na kwamba hivyo ndivyo ilivyo, ni mawazo yanayochukuliwa na watu kadhaa na unaweza kusema kwamba mtu fulani binafsi ana itikadi kama kipengele cha ulinganishi ili kuibua kufanana na kutofautiana kwa itikadi ya msanii mmoja na msanii mwengine.

Watafiti kadhaa ambao wamegusia kipengele cha itikadi katika mashairi ya Kiswahili ni Mulokozi na Sengo (1995), Sengo na Kiango (2012) na Khalfan (2013). Kati ya wataalamu hawa, Khalfan ndiye aliyetafiti kwa kina kuhusu suala la itikadi katika ushairi wa Kiswahili. Akirejelea mashairi ya Saadan Kandoro, Khalfan (2013) anasema kuwa, itikadi ya ujamaa na kujitegemea inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya Saadan Kandoro hususani katika kitabu kiitwacho *Liwazo la Ujamaa* (1968). Katika kitabu hiki yapo mashairi mbalimbali ambayo yanaelezea uzuri wa itikadi ya ujamaa na kujitegemea katika kuwaletea wananchi maendeleo na hivyo kuwataka wanajamii wote kulikubali Azimio la Arusha.

Kwa ujumla, maelezo hapo juu yanabainisha kwamba suala la itikadi linajitokeza katika kazi za fasihi ushairi ukiwemo na hivyo tumeweza kukuza ufahamu na maarifa wetu kuhusu itikadi zinazojitokeza katika kazi za fasihi jambo ambalo limesaidia kusukuma mbele utafiti wetu.

2.5 Itikadi katika Fasihi kwa Ujumla

Itikadi katika kazi za fasihi si kipengele kilichoandikwa na kutafitiwa kwa kiasi kikubwa na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili ikilinganishwa na vipengele vingine vyta maudhui na fani Chuachua (2011). Katika sehemu hii tumeona ni muhimu

kupitia tafiti tangulizi kuhusu itikadi katika fasihi ili kupata mawanda ya namna suala la itikadi lilivyoshughulikiwa na sisi kupata njia ya kusukuma mbele utafiti wetu. Mulokozi (1975), Kezilahabi (1976), Chuachua (2011) na Ambrose (2014), kwa ujumla wao wanabainisha kuwa itikadi ni dhamira inayojitokeza katika riwaya nyingi za Kiswahili kwa sababu hakuna jamii isiyokuwa na itikadi na miiko katika maisha yake ya kila siku. Wanaeleza kwamba kazi za riwaya hubainisha uhalisia wa maisha ambayo ndani yake kuna itikadi za aina kwa aina.

Wafula (2003) amebainisha kuhusu suala la itikadi katika tamthiliya ya Kiswahili, anaeleza kuwa tamthiliya za Kiswahili zinazozungumzia itikadi ni zile ambazo zinaeleza visa na matukio yanayohusisha mashujaa wa kiutamaduni na kihistoria. Tamthiliya anazozitaja katika kuthibitisha hoja yake ni *kinjikitile*, *Mukwava wa Uhehe*, *Mzalendo Kimathi na Kilio cha Haki*. Kimsingi, majina ya tamthiliya hizi yanaonyesha kuwa zinazozungumzia mashujaa kwa sababu hayo ni majina ya watu waliopigana dhidi ya wakoloni ili kukomboa nchi zao na kuzipatia uhuru. Hivyo basi, kwa tamthiliya hizi zinasawiri itikadi walizonazo viongozi hao katika kuzikomboa jamii zao. Utafiti wa Wafula umetusaidia kufahamu kwamba, suala la itikadi linasawiriwa katika kazi mbalimbali za fasihi ikiwemo tamthiliya. Hivyo, katika utafiti wetu tumejikita katika diwani ya *Wasakatonge* kubainisha itikadi zilizojitokeza pamoja na mbinu za kisanaa ambazo zimetumika katika kuibua itikadi.

Mtaalamu Chuachua (2011) ameelezea suala la itikadi kwa kina zaidi katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya za Shaaban Robert namna zinavyosawiri itikadi kama vile, ujamaa na kujitegemea, ubepari, utandawazi, umoja na mshikamano na kufanya kazi kwa bidii. Utafiti wa Chuachua (ameshatajwa) ulijikita katika

kuchunguza itikadi katika riwaya na wa kwetu umejikita kuchambua itikadi katika diwani ya Wasakatonge. Tunachotafiti sisi kipo katika utanzu mwingine tofauti na utanzu wa riwaya uliochunguzwa na Chuachua na pia ni kazi za waandishi tofauti yaani Shaaban Robert na Mohamed Seif Khatib. Hivyo, kazi ya Chuachua imesaidia kusukuma mbele utafiti wetu na kuweza kupata data zilizojibu maswali ya utafiti wetu.

2.6 Pengo la Maarifa

Mapitio mbalimbali yaliyopitiwa hapo juu, yamekidhi haja na madhumuni ya waandishi husika. Hata hivyo, kuna mapengo kadhaa yanayohitaji kuzibwa na utafiti huu kwa sababu tafiti zilizopita hazikushughulikia. Pengo la maarifa lililojitokeza ni pamoja na; mosi, kuchambua masuala ya kiitikadi yanavyojitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge* na pili, kubainisha mbinu za kisanaa zinazoibua masuala ya kiitikadi katika mashairi ya *Wasakatonge* na tatu ni kubaini athari za itikadi hizo kwa jamii.

2.7 Mkabala wa Kinadharia

Katika utafiti huu tumetumia nadharia mbili ambazo ni U-marx na Simiotiki. U-marx umetumika kuchambua masuala ya itikadi katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib na Simiotiki imetumika kuchambua mbinu za kisanaa hususani matumizi ya tamathali za semi katika diwani ya *Wasakatonge* na namna mbinu hizo zilivyoibua itikadi.

2.7.1 Nadharia ya U-Marx

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya U-marx kwa lengo la kutazama mfumo wa maisha ya kijamii kwa kuzingatia hali ya mazingira ya jamii. Katika jamii kuna

matabaka na ni katika matabaka hayo ndimo mahusiano ya kijamii huzaliwa, kujengwa na kukuzwa (Eagleton, 1977).

U-Marx ni nadharia iliyopata umaarufu mkubwa katika tasnia ya taaluma mnamo karne ya kumi na tisa katika bara la Ulaya na baadae kusambaa duniani kote. Mwasisi wa nadharia hii ni Karl Marx aliyezaliwa mwaka 1818 huko Ujerumani na kufariki mwaka 1883 akiwa na umri wa miaka 65 (Mehring, 1962). Mnamo mwaka 1836 alihitimu shahada ya uzamivu katika chuo kikuu cha Berlin ambapo ndipo alipoanza kuandika maandiko na machapisho ya makala mbalimbali katika magazeti.

Nidhahiri kuwa, moja ya mambo ambayo aliyokuwa anaandika ni kukosoa serikali na mfumo wa kubepari kwa msingi kwamba ilikuwa ni mfumo wa kinyonyaji kwa matajiri kuwanyonya watu maskini (Bell, 1977). Hata hivyo, hakuweza kuendelea kuikosoa serikali na mfumo wa kibepari kwani alifukuzwa Ujerumani na kuhamia ufaransa ambako nako pia alifukuzwa na kwenda kuishi London (Mehring, 1962).

Linebaugh (1976) anasema kwamba, nadharia ya U-Marx inafafanua kuwa ili kuleta usawa katika jamii ni lazima kuondosha ubepari na kuanzisha itikadi ya ujamaa ambayo inaitaka serikali kuwa ndiye mmiliki wa nyenzo za uzalishaji mali badala ya umiliki binafsi kama ilivyo katika ubepari. Karl Marx anaamini kuwa nyenzo za uzalishaji mali kama ardhi, mitaji, ujasiriamali na nguvu kazi zikiwa zinamilikiwa na mtu mmojammoja kamwe haziwezi kuitoa jamii katika mfumo wa unyonyaji. Hali hii huifanya jamii kuwa na watu wengi ambao ni maskini sana na watu wachache kuwa matajiri sana (Marx na Engels, 1848).

Nadharia hii hujishughulisha na tabaka la kiuchumi na sababu za kiitikadi zinazotawala jinsi mtunzi anavyofikiria na kuandika akizingatia uhusiano wa kazi ya fasihi na uhalisia wa jamii uliopo wakati huo, hujihusisha pia na mtazamo wa uhalisia wa kijamii wa wakati kazi ilipotungwa. Nadharia hii huzingatia maudhui katika kazi ya fasihi kwa kuangalia uhakiki wa kimaadili, na njia za kuyaboresha maisha ya jamii iliyoshughulikiwa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2006), Umarx ni falsafa ya kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu, ikimaanisha kwamba mawazo yake hayategemezi kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali yanategemeza kwenye uhalisia unaoonekana.

Nadharia hii ilianzishwa na Karl Marx mwaka 1818-1862 na Fredrich Engles mwaka 1820-1895. Katika nadharia hii Marx amejikita katika historia na miundo ya kijamii kwa kupitia hoja kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kueleweka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo inachunguza njia mbalimbali za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi ambayo huathiri uzalishaji na usambazaji wa mali hizo. Hivi vyote kwa pamoja huunda misingi ambapo kwenye misingi hiyo huunda maadili, itikadi, dini na utamaduni.

Upungufu katika nadharia hii unajitokeza katika kuchagua kiwango au namna ya maisha kitakachoizingatiwa kwani ni vigumu kwa kazi ya fasihi kuzingatia maisha ya jamii katika ujumla wake (Ntarangwa, 2004). Kwa mfano ikiwa mtunzi atachagua kuonesha starehe na furaha ya maisha ya tabaka tawala bila kuonesha uchochote wa tabaka linalotawaliwa, atakuwa kakiuka msingi ya kutoa picha halisi ya maisha

katika jamii. Pia, katika utafiti huu, nadharia hii si muafaka katika kuchunguza vipengele vya kifani katika kazi ya fasihi kwa kuwa mtazamo na mawazo yake makuu yamejikita katika dhamira pekee yake. Katika utafiti huu, baada ya kubaini mapungufu hayo tulilazimika kuwa na nadharia nyingine ambayo ilitusaidia katika uchambuzi wa matumizi ya lugha ya tamathali za usemi katika diwani ya *Wasakatonge*.

2.7.2 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni nadharia inayohusu taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha (Nazarova, 1996). Simiotiki ni neno la kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumwiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi ambazo zinaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002). Ishara inajitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia mazingira ya jamii, kiuchumi, kisiasa na hata kiutamaduni.

Mark (1995) anaeleza kuwa watanzi wa kazi za fasihi hutumia lugha ya picha na ishara kwa kutumia alama ambazo zinafahamika kwa urahisi na wanajamii wanaoandikiwa kazi hiyo ya fasihi. Kwa mfano, watanzi wa kazi za fasihi huweza kutumia wanyama, wadudu, miti, mizimu, mashetani, na mawe na kirejelea matendo na tabia za mwanadamu, kwa nia ya kuifunza jamii masuala muhimu katika maisha.

Wamitila (2002) anasema kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja yaani, umbo ambalo alama inachukua na kirejelee yaani, maana iwakilishwayo na alama hiyo. Katika maelezo hayo tunapata picha kwamba kuna kitaja na kirejelee,

vitu hivyo jamii inakuwa imekwisha kubaliana katika mawasiliano yao. Mfano katika jamii ya watu wa pwani neno kuvunja ungo lina maana kubwa sana kwao. Neno hilo halina mahusiano kabisa na kuharibu kifaa cha kitamaduni cha kupepetea mahindi au kuchagulia mchele, bali wanajamii wa jamii hiyo wanaelewa maana yake. Neno kuvunja ungo msanii anaweza kulitumia awezavyo ili kuweza kujenga picha, ishara na taswira mbalimbali katika kazi yake.

Barthes (1994) anaeleza kwamba, kuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Simiotiki: Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, kihemenitiki, kisema, kiishara na kiutamaduni: tunaposoma kazi za fasihi tunakutana na matumizi ya lugha ambayo yanajenga misimbo ya aina hizo tano. Kwa mfano, msimbo wa kimatukio hujitokeza, kwa mtunzi wa kazi ya fasihi kujenga tukio linalofanywa na wanyama kama vile mbwa, fisi, paka na ng'ombe ambapo kwa msomaji huweza kujenga taswira, ishara na picha ambazo zitampatia dhamira stahiki.

Msimbo wa kiheminitiki; msimbo huu unatokana na anuani ya kifasihi kama jina la kitabu, jina la shairi, kichwa cha igizo/onesho au jina la suara katika riwaya (Mark, 1995). *Wasakatonge* ni jina la kishairi ambao inatupa picha fulani ya kufahamu maudhui ambayo yanapatikana katika mashairi ya wasakatonge. Msimbo wa kihemenitiki husaidia katika kujenga tataruki kwa wasomaji kwani wanapokutana na jina la diwani kama *Wasakatonge* hujiliza maswali mengi kwa wakati mmoja kuhusu kuna nini kinachozungumzwa kuhusu *Wasakatonge*.

Msimbo wa kiseme; neno seme hutumiwa kuelezea elementi nasibishi ya kisementiki. Sementiki ni taaluma inayoshughulikia maana za maneno katika lugha

ya mwanadamu. Katika taaluma ya semantiki maneno huwa yanakuwa na maana ya msingi na maana ya ziada. Maana ya msingi ya neno ni ile ambayo inaweza kutumika na kurejelewa katika muktadha rasmi wakati maana za ziada za neno zinaweza kurejelewa katika muktadha usiokuwa rasmi. Msimbo wa kiseme katika taaluma ya fasihi hutumiwa na wanafasihi kujenga dhamira na maudhui kwa kutumia maneno ambayo yanatoa ukaribu wa maana ya msingi ya neno na kile kinachorejelewa na neno hilo la kifasihi (Wright, 1975). Katika utafiti huu tumetumia msimbo huu katika kuchambua matumizi ya lugha ya sitiari, tashibiha, tashihisi na kejeli kama zinavyojitokeza katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib katika mashairi yake ya *Wasakatonge*.

Msimbo wa kiishara; matumizi ya lugha ya ishara yanatumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kwa kiwango kikubwa (Senkoro, 2006). Hii inatokana na ukweli kwamba, kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya jamii kwa kutumia lugha ya picha na ishara na kasha kuyawasilisha kwa jamii. Msimbo wa kiishara wa nadharia ya Simiotiki humsaidia mtatifi au mhakiki wa kazi ya fasihi kuweza kubainisha lugha ya ishara iliyotumika katika kazi ya fasihi na kuweza kusema hapa kuna dhamira fulani.

Mathalani katika utunzi wa Mohammed Seif Khatib katika mashairi ya *Wasakatonge*, tumeona namna akiwasilisha kazi ya fasihi kwa kusawiri maisha halisi ya nchi zetu za Afrika Mashariki hususani nchi ya Tanzania kwa kuonesha namna ya kufikia ujenzi wa jamii mpya kwa kuondokana na ukoloni mamboleo, kupiga vita kumomonyoka kwa maadili katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, kuwa na mapenzi ya dhati katika ndoa, na kadhalika.

Msimbo wa kiutamaduni; watanzi wa kazi za fasihi hutumia viashiria vya utamaduni katika kazi zao wakiwa na nia ya kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa wasomaji. Mathalani, katika mashairi ya *Wasakatonge* tunaona mtunzi akitumia msimbo wa kiutamaduni kwa kubainisha namna wanawake wanavyotakiwa kujikombua kuondokana na uonevu na unyanyasaji wa kijinsia, kwani kwa itikadi au mtazamo wa jamii katika nchi za Afrika wanawake wanaonekana viumbe dhaifu na wasio na mchango wowote katika jamii zao, katika “*Shairi la Wanawake*” (uk 16) hivyo basi, kupitia msimbo wa kiitamaduni tunapata dhamira ya ukombozi inayobainisha ni namna gani wanawake wa Bara la Afrika wanavyotakiwa kujinasua katika dimbwi la unyanyasaji na kujisimamia wao wenyе bila kupata usaidizi wa yejote.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, udhaifu mkubwa wa nadharia ya Simiotiki unatokana na msisitizo wake mkubwa kwenye lugha na sifa nyinyine zinazoonekana ndogo badala ya kujihusisha na fasihi kwenye upana wake. Katika utafiti huu, nadharia hii iliteuliwa kwa sababu mihimili yake mitano ilionekana kufaa katika kutimiza lengo la msingi la utafiti wetu, hivyo basi, nadharia hii ilibainishwa kama kijazilizi cha nadharia ya Umarx katika uchunguzi, uchambuzi na mjadala wa data na matokeo ya kazi hii. Katika utafiti huu, nadharia ya Simiotiki imetumika kuchambua matumizi ya lugha ya tamathali za semi katika mashairi ya *Wasakatonge* ili kutimiza dhununi mahususi la utafiti.

Kimsingi, uteuzi wa nadharia mbili katika utafiti huu umefanywa ili kuweza kujaziliza pengo au mapungufu ya nadharia moja katika kuchambua, kuchunguza na kujadili data za utafiti. Katika kufikia malengo ya utafiti huu kila nadharia ilionekana

kuwa na msingi thabiti katika kukidhi malengo. Hivyo basi, nadharia zote mbili zimetumika katika kukidhi malengo ya utafiti huu kwa kujazilizana na kutegemeana.

2.8 Hitimisho

Sura hii imewasilisha dhana ya ushairi kwa jumla na ushairi wa Kiswahili, mapitio kuhusua masuala ya kiitikadi katika kazi za fasihi hususani ushairi wa Kiswahili, mapitio kuhusu mashairi ya Mohammed Seif Khatib kwa mujibu wa wataalam mbalimbali, mapengo yanayojiteza na mikabala ya kinadharia ambayo ni nadharia ya U-maarx na nadharia ya Simiotiki zilizotumika katika kuchambua, kujadili data na matokeo ya kazi ya utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusu vipengele vya usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data, uhalali na uthabiti wa utafiti na maadili ya utafiti.

3.2 Usanifu Utafiti

Usanifu wa utafiti ni ramani kamili ambayo inaonesha namna utafiti husika utakavyokuwa tangu mwanzo mpaka mwisho (Kothari, 2008). Utafiti huu umeteua usanifu wa uchunguzi kifani ambapo katika aina hii ya usanifu, mtafiti huteua kitu au jambo maalumu la kulifanya utafiti. Uchunguzi kifani katika utafiti wetu ni diwani ya *Wasakatonge* ambapo tunachunguza masuala ya itikadi ndani ya diwani hiyo. Katika kuhakikisha lengo kuu la utafiti linakamilika, data za utafiti huu zimekusanywa na kuchambuliwa kwa mkabala wa kitaamuli. Mkabala wa kitaamuli unaruhusu matumizi ya tafakuri katika kuhusisha taarifa za utafiti na kisha kuzitolea ufanuzi kwa misingi ya nadharia husika (Enon, 1999; Kothari, 2008). Mbinu ya uchunguzi kifani ni nzuri kwa sababu humuwezesha mtafiti kukusanya data nyingi kwa muda mfupi kwa sababu tayari ameshafahamu data za utafiti wake anazipata wapi na hivyo kutopoteza muda kwenda kwenye vitu vingine ambavyo havihuiani na utafiti wake. Mkabala wa kitaamuli nao ni muafaka katika utafiti huu wa kifasihi ambapo uchambuzi wa data umefanywa kwa kutolewa maelezo ambayo yanasaidia kujibu maswali ya utafiti.

3.3 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo utafiti umefanyika kulingana na vile mtafiti anavyopendekeza ili kupata data za kujibu maswali ya utafiti (Cresswell, 2009).

Eneo la utafiti huteuliwa kulingana na nia kuu ya mtafiti na kwamba eneo au maeneo ambayo yanateuliwa ni lazima yaweze kutoa data za kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti. Utafiti huu ni wa kifasihi na data zake zimekusanya kutoka katika diwani ya *Wasakatonge* na hivyo ilihitajika eneo maalumu ambapo mtafiti anataweza kujisoma diwani hiyo kwa utulivu ili kuweza kupata data za utafiti. Hivyo mtafiti aliteua maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Manyara ambapo aliweza kupata nafasi ya kuisoma kwa makini diwani husika na kukusanya data zilizohitajika katika utafiti huu.

3.4 Sampuli na Usampilishaji

Kipengele hiki kinahusu sampuli na usampulishaji na namna itakavyopatikana sampuli ya utafiti.

3.4.1 Sampuli

Sampuli ni sehemu ya watafitiwa ambayo inateuliwa kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kuwa ni kiwakilishi cha kundi nzima katika utafiti (Yin, 2001).

Sampuli ya utafiti huteuliwa kwa sababu ni vigumu kwa mtafiti kuweza kuwatafiti wanajamii wote au wango yote, hivyo anateua sehemu ya wango na kuitumia kupata data za utafiti. Sampuli ya utafiti huu ni diwani moja inayofahamika kwa jina la *Wasakatonge* iliyoandikwa na Mohammed Seif Khatib. Tumeiteua diwani hii ili kuweza kupata data za utafiti kulingana na madhumuni mahususi ya tasinifu hii. Mohammed Seif Khatib ameandika kazi kadhaa za mashairi kama vile *Malenga*

Wapya, Ukombozi wa Zanzibar (1975), Pambazuko la Afrika (1982), Fungate ya Uhuru (1988), na Taarab Zanzibar (1992), lakini sisi tumeteua diwani ya *Wasakatonge* kwa sababu ndiyo ambayo inaweza kutupatia data za utafiti huu kwa mujibu wa malengo mahususi ya utafiti.

3.4.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo inahitajika katika utafiti husika. Katika utafiti huu tumetumia mbinu ya usampulishaji lengwa ambayo huruhusu uteuzi wa watafitiwa wale wanaofaa tu katika utafiti husika (Babbie, 1999). Usampulishaji lengwa ni mbinu ya kuteua sampuli kwa makusudi mtafiti akiwa na imani kwamba sampuli hiyo itampatia mtafiti data anazohitaji katika kutimiza madhumuni mahususi ya utafiti wake. Hivyo, tumeiteua diwani ya *Wasakatonge* kwa makusudi tukiwa na imani kwamba itasadia kutoa data ambazo zinahusiana na masuala ya itikadi kama madhumuni mahususi yanavyojieleza.

3.5 Data za Utafiti

Utafiti huu umekusanya data za msingi na taarifa za upili ambazo zimetumika katika kushadadia data za msingi. Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hakuna mtafiti mwengine yeoyote ambaye amewahi kukusanya data kama hizo kwa madhumuni kama ya utafiti uliofanyika na kuandikwa tasinifu hii. Hivyo, data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika diwani ya *Wasakatonge* zikihusisha masuala ya itikadi na mbinu za kisanaa zilizotumika kuibua masuala hayo ya kiitikadi katika diwani hiyo. Taarifa fuatizi hizi ni zile ambazo tayari zipo katika maktaba kuptitia machapisho kama vitabu, majarida,

makala, magazeti, ripoti na tasinifu. Taarifa hizi hukusanya na mtafiti ili kuweza kushadadia hoja zimeibuliwa na data za msingi.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data na Taarifa za Upili

Data za utafiti huu zimekusanya kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na taarifa za upili zimekusanya kwa kutumia mbinu ya upitiasi wa nyaraka.

3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data kutoka katika matini kwa lengo la kupata data za msingi ambazo zitasaidia katika kujibu maswali ya utafiti husika (Kombo na Tromp, 2006). Tofauti na mbinu nyingine za kukusanya data za msingi uwandani, mbinu hii humtaka mtafiti pamoja na wasaidizi wake kuandaa muongozo wa kukusanya data kutoka katika matini ili kuweza kutimiza madhumuni mahususi ya utafiti wake. Kimsingi, data za utafiti huu zimekusanya kutoka katika diwani ya *Wasakatonge* ambapo mtafiti aliisoma diwani hiyo zaidi ya mara tatu kabla ya kuanza kukusanya data kwa kuzingatia hatua kadhaa ambazo zimeelezwa vizuri katika kiambatanisho namba 1.

3.6.2 Upitiasi Nyaraka

Upitiasi wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya taarifa za upili ambazo ni muhimu katika kujazilishia data za msingi za utafiti husika. Mtafiti alilazimika kukusanya taarifa za upili kwa lengo la kuthibitisha na kushadadia hoja zitokanazo na data za msingi. Pia, mbinu hii ilitumika ili kupata maarifa zaidi kuhusiana na nadharia zilizoteuliwa kuongoza utafiti huu na namna ya kuzitumia nadharia hizo katika kuchambua data. Upitiasi wa nyaraka umehusisha matini ambazo zinapatikana katika maktaba kama

vitabu, tasinifu, makala, majarida, magazeti, ripoti na maandiko mengine ambayo bado hayajachapishwa lakini yanahusiana na mada ya utafiti.

3.7 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kama inavyofafanuliwa hapa chini.

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Data za utafiti huu zimewasilishwa na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kama ilivyoahidiwa katika usanifu wa utafiti. Mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya kuchambua data kwa kuzitolea ufanuzi wa maelezo ambao hauhusishi hesabu (Aronson, 1992). Data za utafiti zimewasilishwa kwa madondoo kutoka katika diwani ya *Wasakatonge* kulingana na itikadi husika na kisha kuchambuliwa kwa maelezo ambayo yanasaidia kujibu maswali ya utafiti na kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti huu. Maelezo ya hatua zilizozingatiwa katika ukusanyaji wa data yanapatikana katika kiambatanisho namba 2.

3.8 Usahihi wa Data

Usahihi wa data, ni utaratibu anaoutumia mtafiti katika upatikanaji wa data sahihi na za kuaminika (Cohen na Wenzake, 2000). Katika kuhakikisha upatikanaji wa data sahihi za utafiti wetu, tumetumia mbinu ya usomaji makini katika kukusanya data na mbinu ya upitiaji wa nyaraka katika kukusanya taarifa za upili. Mbinu hizi ni muafaka kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti huu na hivyo data zilizokusanywa ni sahihi na zimesaidia kutimizwa kwa madhumuni mahususi ya utafiti huu.

3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ya utafiti ni mojawapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, akitekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake (Robson, 2007). Miongoni mwa mambo muhimu ambayo anatakiwa mtafiti kuyazingatia ni suala la maadili. Maadili yanayotakiwa kufuatwa na kuzingatiwa ni kama vile kupata kibali cha kufanya utafiti, kutunza siri za watafitiwa, kuheshimu mipaka ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data. Katika utafiti wetu tumezingatia maadili hayo ili kupata data sahihi katika kazi yetu.

3.10 Hitimisho

Sura hii inayohusu mbinu za utafiti ni muhimu sana katika utafiti kwa sababu ndiyo inayoonesha usayansi wa kufanyika kwa utafiti husika. Mbinu za kukusanya, kuchambua data na vipengele vingine muhimu katika kuwezesha kupatikana kwa data sahihi na muafaka katika utafiti huu vimewasilishwa katika sura hii. Vipengele hivyo ni pamoja na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya na kuchambua data, usahihi wa data na uzingativu wa maadili ya utafiti. Sura inayofuata ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji, uchambuzi, na mjadada wa data za utafiti. Sura hii inaongozwa na malengo mahususi ya utafiti ambayo ni kubainisha masuala ya kiitikadi yanayojitokeza katika diwani ya Wasakatonge na kuelezea mbinu za kisanaa ambazo zinatumika kuibua itikadi katika diwani ya Wasakatonge. Katika kufanya uchambuzi wa data za utafiti wetu tumeona ni vema tuanze kueleza historia ya mtunzi Mohammed Seif Khatibu ili wasomaji waweze kumwelewa yeýé ni nani na kisha waweze kuunganisha uchambuzi wa data na mjadala pamoja na historia yake.

4.2 Historia ya Mshairi Mteule Mohammed Seif Khatib

Mohammed Seif Khatib ni mtunzi wa kazi za fasihi hususani ushairi. Mohammed Seif Khatib alizaliwa mnamo mwaka 1951 katika kijiji cha Umbuji nchini Zanzibar na alifanikiwa kuwa mwalimu katika maisha yake akisomea katika chuo cha Nkrumah, Zanzibar. Baada ya kusomesha kwa muda, akajiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuhitimu shahada ya B.A Ed. katika fani ya fasihi, isimu na taaluma ya maendeleo na ualimu mwaka 1978. Mwaka 1982 alitunukiwa shahada ya M.A. katika Chuo Kikuu cha London. Mohammed Seif Khatib ni mwanasiasa, mwandishi mahiri na mshairi razini. Baadhi ya vitabu vyta ushairi na kazi za fasihi wa mtunzi huyu, ni *Wasakatonge* (2003) pamoja na *Ukombozi wa Zanzibar* (1975), *Pambazuko la Afrika* (1982), *Fungate ya Uhuru* (1988) na *Taarab Zanzibar* (1992), na “Chanjo na Matakwaa ya Mwanaume katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho

wa Ushairi wa Muyaka Bin Haji na Shabaan Robert,” Tasnifu ya Uzamivu Chuo Kikuu Cha Dodoma (2011).

Huyu ndiye mwandishi Mohammed Seif Khatib ambaye amewahi kuwa kiongozi wa chama cha mapinduzi katika ngazi mbalimbali, mbunge na waziri katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mpaka umauti unamkuta mwaka 2021, Mohammed Seif Khatibu alikuwa ni mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA). Mwandishi huyu ameacha utajiri mkubwa wa fasihi ya Kiswahili ambapo leo Watanzania na wapenzi wote wa lugha na fasihi ya Kiswahili wanajivunia utajiri huo wa kazi za fasihi za nguli huyu na ndiyo maana tukaamua kufanya utafiti wa kuchunguza masuala ya itikadi katika diwani yake ya *Wasakatonge*.

4.3 Itikadi katika Diwani Teule

Madhumuni mahsusini ya utafiti huu yalikuwa ni kuchambua masuala ya kiitikadi yanayojitokeza katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib katika diwani ya *Wasakatonge* na kubainisha mbinu za kisanaa zinazoibua masuala ya kiitikadi. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia ya usomaji makini ambapo mtafiti alisoma diwani teule kwa makini na kuweza kupata data za utafiti kama ilivyoelezwa katika sura ya tatu ya tasinifu hii. Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti ni kama ifuatavyo:

4.3.1 Itikadi Zinazojitokeza katika Diwani ya *Wasakatonge*

Karl Marx (1977) katika *The German Ideology* anasema kuwa, Itikadi ni fikra zote ambazo msingi wake ni mfumo wa uzalishaji mali na teknolojia. Hujumuisha maoni ya binadamu kuhusu anayoyasema na anayoyafikiria katika siasa, sheria, maadili,

dina na falsafa. Mawazo hayo hugeuka pindi mfumo huu unavyobadilika, hivyo itikadi na jamii huendelea kubadilika. Itikadi ndio ambayo hueleza na kuhalalisha mfumo wa siasa na kiuchumi wa jamii. Mtaalamu huyu aliona itikadi kama ung'amuzi potoshi yaani imani ya uongo. Anafanananisha itikadi ya kidini ambayo hutumiwa na mifumo ya kibepari na ukabaila kuwafanya watu waamini viongozi humwakilisha Mungu, kila mtu ana nafasi yake ambayo Mungu amemratibia.

Katika kuchunguza masuala ya kiitikadi katika mashairi ya *Wasakatonge*, utafiti umeweza kubaini kuwa mtunzi ameweza kuibua masuala ya itikadi za aina mbalimbali kama vile itikadi ya kupiga vita uongozi mbaya, kuwa na demokrasia ya kweli na utu, ukoloni mamboleo, matabaka katika jamii, unafiki na usaliti katika jamii, kufanya kazi kwa bidii, mmomonyoko wa maadili katika jamii, hali ngumu ya maisha, ukombozi wa; kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kifikira/mawazo na kimapenzi na nafasi ya mwanamke katika jamii na itikadi ya kidiplomasia.

4.3.2 Itikadi ya Kupiga Vita Uongozi Mbaya

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004) inasema kwamba, Uongozi ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia shughuli au asasi. Kwa mantiki hiyo, uongozi mbaya tunaweza kusema ni matumizi mabaya ya madaraka. Chuachua, (2011) anasema kwamba itikadi ni imani au mtazamo alionao mtu kuhusu maisha kwa ujumla wake, hususani katika kufanikiwa ama kutofanikiwa katika maisha. Katika utafiti huu tulibaini itikadi na shauku ya mtunzi ya kutaka kuingia katika mapambano ya ujenzi wa jamii mpya kwa ari kubwa ya kuihiza jamii husika kupiga vita uongozi mbaya ambao ni kikwazo cha kufikia ujenzi wa jamii mpya. Muhammed Seif Khatib anasema kwamba suala la uongozi mbaya linaonekana kuwa

ni tatizo kubwa katika Bara la Afrika kwani viongozi wetu wengi wanaongoza kwa kutumia mabavu na kama jamii haitatafuta tiba basi tutaendelea kuwa na machafuko ya kisiasa na vita vya wenyewe kwa wenyewe kila wakati. Hii inadhihirisha katika shairi la “*Madikteta*” (uk, 21) kwamba,

*Mizinga hiyo mitutu,
Haitoi risasi,
Hutoa maraisi,
Walio madikteta.*

Ni dhahiri kuwa, nchi nyinyi za Bara la Afrika zimekosa maendeleo kutokana na viongozi wengi kutumia mabavu na nguvu kwani ukichunguza katika shairi hilo utaona namna mwandishi anawasilisha itikadi ya uongozi mbaya ambapo upo katika jamii yake. Anaonyesha namna mizinga na mitutu iliyobeba risasi inavyotumika kupata na kulinda viongozi wabaya katika jamii jambo ambalo linapelekea maendeleo kukoseakana. Na katika shairi la “*Nahodha*” ubeti wa tatu mtunzi anasema kwamba,

*Nahodha,
Wang’ang’ania sukani,
Abiria, sote tunateseka,
Teseka, kulewa na kutapika,
Kutapika, na ngama inatutoka,
Inatutoka, vikongwe vyasulubika,
Sulubika, mama vyataabika,
Nahodha tosa nanga!*

Hapa mtunzi anaonyesha jinsi baadhi ya viongozi katika Bara la Afrika hushindwa kuongoza nchi zao na wanapotakiwa kuwajibika kwa wananchi kwa kujiuzulu huwa hawakubali jambo ambalo hupelekea nchi nyingi kuingia katika machafuko

makubwa kwa wananchi wenyewe kutumia nguvu ya umma kuwaondoa madaraka viongozi wa baya. Hili tumeweza kulieleza vizuri kwa kuongozwa na nadharia ya U-marx ambapo katika dondoo tumeona kuna kundi la watawala na wataliwa na pia nadharia hii ya U-Marx ambayo imetusaidia kuelewa kwamba “Nahodha tosa nanga” maana yake ni kumtaka kiongozi kujiuzulu jambo ambalo limekuwa gumu kwa viongozi wa Kiafrika kukubali kulitekeleza.

4.3.3 Itikadi ya Demokrasia ya Kweli na Utu

Katika kushughulikia suala la demokrasia katika nchi za Bara la Afrika hususani katika Afrika Mashariki, yapo baadhi ya mashairi ya watunzi kama vile Abdilatif Abdalla, “*Sauti Dhiki*” (1988), Alamin Mazrui, *Chembe cha Moyo* (1988) na Said Ahmed Mohammed, *Jicho la ndani* (2002) ambayo yamezungumzia demokrasia katika vipengele vya; siasa, rasilimali ya taifa, uhusika katika masuala ya utawala wa taifa, uhuru wa kutoa maoni au kujieleza na haki ya kuwapo kwa vyama vingi katika taifa. Katika nchi ambayo inazingatia demokrasia, kila mtu ana haki ya kubainisha fikra zake pasi na kuwekewa vikwazo (Njogu na Chimerah, 1999). Fikra hizo kama maoni, huweza kuwa za kukashifu utawala wa nchi uliopo kwa malengo ya kuelekeza, Kezilahabi (1977). Iwapo utawala wa nchi hautoi fursa hiyo kwa raia wake ili kutoa mawazo ya kuchangia namna utawala unavyoweza kuendeshwa; wanaotoa mchango huo huweza kusingiziwa kuwa ni wachochazi na wasaliti. Kadhalika, demokrasia ni dhana pana inayoangaliwa katika miktadha ya kiliberali na kijamii. Wanauliberali wanaeleza demokrasia kama ni uhuru alionao mtu mmojammoja katika jamii wa kufanya chochote atakacho bila kuvunja sheria za nchi. Vilevile, demokrasia ni uhuru na haki ya kushirikishwa katika maamuzi

mbalimbali yanayohusu maendeleo binafsi na taifa kwa ujumla (Mpangala, 1977; 2004). Kwa mazingira hayo ni dhairi kuwa ushairi wa Kiswahili unatoa mwanya katika utafiti huu kwani tumbaini kuwa mtunzi wetu Mohammed Seif Khatib amewasilisha itikadi ya kuwa na demokrasia ya kweli na utu katika jamii kwa kuonyesha kuwa katika nchi nyingi duniani hususani bara la Afrika suala la demokrasia ya kweli hakuna. Kukosekana kwa demokrasia ya kweli husababisha utu kutoweka mionganini mwa viongozi na wanajamii. Katika shairi la “*Saddam Hussein*” (uk 26-27) na “*Unyama*” (uk 47-78) mtunzi amebainisha namna viongozi wanavyo ongoza nchi zao bila kujali utu kwa kuwafanya raia wao mambo ambayo ni kinyume kabisa na haki za kibinadamu. Katika shairi la “*Unyama*” ubeti wa pili na wa tatu anasema kuwa:

*Binadamu dikiteta,
Na nchi huzitawala,
Kwa mbinu na kwa hila,
Ni mkandamzaji.*

*Binadamu ana vyombo,
Amejenga mahakama,
Polisi chungu nzima,
Na jeshi la kuandama,
Kuadhibu “wakaidi”.*

Hapa ni dhahiri kwamba mtunzi ameonyesha itikadi ya kidemokrasia kwa kujali utu kwa kuhimiza viongozi na jamii kujali utu wa mtu na kuachana na ubinafsi wa viongozi kujali utu wao tu na kuwasahau wananchi maskini wanaowaongoza na kwa kufanya hivyo wadumishe demokrasia ya kweli kwani ndio msingi imara utakayesaidia kuleta maendeleo ya kweli na kujenga jamii mpya yenye usawa kwa

wote. Nadharia ya U-marx inatusaidia kubaini kwamba katika ubeti wa pili kunaonekana dhana ya kuwepo kwa matabaka ambapo viongozi wanatumia hila kuingia madarakani bila ridhaa ya wananchi amba ni wengi. Pia, katika ubeti wa tatu nadharia hii ya U-marx tunaioma ikijitokeza pale ambapo viongozi wameamua kuandaa vyombo vyta dola kama mahakama, jeshi na polisi kwa ajili ya kuwashughulikia wote amba wanadai demokrasia lakini hapa wanaitwa ni “wakaidi.” Jambo la msingi ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata uhuru wa kutoa maoni yao na pia kuchagua viongozi wanaowataka kwa uhuru.

4.3.4 Itikadi ya Ukoloni Mamboleo

Nyerere (1968) anasema kwamba, binadamu wote ni sawa, kila mtu anastahili heshima, kila mtu anahaki ya kupata hifadhi ya maisha yake na ya mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria, kila mmoja anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake. Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao. Vile vile, katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakwenda sawa, serikali lazima iwe na mamlaka kamili juu ya njia muhimu za kukuza uchumi. Pia serikali iweze kutumia mali yote ya nchi katika kuondoa umaskini, ujinga na maradhi.

Katika uchunguzi wa utafiti huu tumebaini kuwa mtunzi anaonyesha kuwa itikadi ya ukoloni mamboleo kwani imekuwa kikwazo kikubwa katika kufikia ujenzi wa jamii mpya katika nchi nyingi za Afrika kwani fikra za utegemezi kwa wananchi zinaathiri jamii katika suala zima la maendeleo katika nyanja zote muhimu za kiuchumi, kisiasa na utamaduni kwa ujumla.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa, nchi nyingi za Afrika zinategemea bado misaada toka nje na hufanya nchi hizo kudumaa na kuwa wategemezi katika mitaji, dawa, mashine, pembejeo pamoja na teknolojia katika shairi la “*Wafadhiliwa*” (uk 38) ubeti wa kwanza mtunzi anasema kuwa:

Wafadhiliwa kufurahishwa,

Será zao kupitishwa,

Rais anaamrishwa,

Tekeleza!

Taifa linadhalilishwa,

Mambo mengi kushurutishwa,

Na bila kushirikishwa,

Yaoneni!

Uhuru wetu twauuza,

Na heshima tunapoteza,

Historia itatubeza,

Amkeni!

Katika shairi la “*Hatua kali*” (uk 8-9) na “*Tiba isiyotibu*” (uk 18) mtunzi anaonyesha kabisa namna misaada inayotolewa na wahisani inavyokuwa na masharti magumu jambo linaloweza kupelekea nchi zetu kutawaliwa kiuchumi na nchi inayotoa misaada pindi nchi husika inaposhindwa kulipa madeni au kutimiza masharti yao. Hivyo basi mtunzi anaiasa jamii yake iwe makini na kuachana na fikra za ukoloni mamboleo kwani kwa kuendelea kuishi kwa mtazamo wa kutegemea wahisani itafanya nchi zetu kuishi bila uhuru kamili katika nyanja za kiuchumi na kisiaza jambo ambalo litakwamisha kufikiwa kwa ujenzi wa jamii mpya. Mfano katika shairi la “*Hatua kali*” mtunzi anasema kuwa:

*Maagizo tunapewa,
Mipango tunapangiwa,
Na amri tunatolewa.*

*Será zote siyo zetu,
Zimeletwa huku kwetu,
Hazina faida katu.*

Kwa ujumla mtunzi katika mashairi hayo ameendelea kubainisha, namna wahisani wanavyotupatia maagizo, mipango, sera na misaada yao ambayo haina faida kwa wananchi. Nadharia ya U-marx inatuwezesha kupata uelewa kwamba nchi za Kiafrika zinaonekana kuwa ni za tabaka la chini na zile za Ulaya na Marekani ni tabaka la juu ambalo linazipangia nchi za Afrika mambo ya kufanya. Nchi zinapopangiwa mambo ya kufanya zinakuwa tegemezi kwa sababu mipango ya maendeleo haijatokana na wananchi wanchi hizo. Katika hali ya kawaida ni vigumu sana kutekeleza mpango wa maendeleo wa kupangiwa na mtu au taifa jingine. Mipango ya maendeleo hupangwa kulingana na mazingira ya nchi husika na wahusika wenyewe. Itikadi ya utegemezi ni mbaya sana na inaweza kuifanya jamii kuwa duni licha ya kuwa na rasilimali nyingi za kuwaletea maendeleo. Kwa kuzingatia mawazo ya nadharia ya U-marx ni kwamba elimu inapaswa kutolewa ili kuiwezesha jamii kufahamu athari za utegemezi na kuamua kufanya kazi kwa kujitegemea wao wenyewe.

4.3.5 Itikadi ya Matabaka katika Jamii

Akieleza kuhusu matabaka katika jamii, Marx (1979) katika *Pre-Capitalist Social Economic Formation* anasema kwamba, historia ya jamii zote ni mapambano ya matabaka mbalimbali. Anaendelea kueleza kuwa uhusiano baina ya fasihi na

uzalishaji mali kama vile mapinduzi yanayofanyika na kufaulu, mfumo wa uzalishaji mali hubadilika na taasisi zote za kiutamaduni huchukua mkondo mwingine. Anasema kuwa, wanadamu daima huwa katika harakati za kufanya hali yao kuwa bora zaidi na ili mapinduzi yafanyike huwa na hatua tatu kihistoria. Hatua hizi ni pamoja na ile ya wanadamu kuiishi kwa pamoja na kufaidi jamii ambayo inafahamika kama ujima. Hatua ya pili ni biashara ndogondogo iliyoendeleza na kukuza tabaka la wafanyakazi na baadaye hatua ya tatu ambayo ni jamii kufikia katika mfumo wa kibwanyenye na kibeberu uliotokana na dhuluma za wafanyakazi kwa malengo ya mabeberu.

Katika diwani ya *Wasakatonge* mtunzi amebainisha namna suala la matabaka yanavyojitokeza katika jamii yake kwa kutumia shairi la “*Kansa*” (uk 4) kwa kusema kuwa yapo matabaka mawili katika nchi zetu za Kiafrika yaani tabaka la juu (tawala) na tabaka la chini (watawaliwa/wasionacho). Mtunzi ametumia shairi la *kansa* kwa kusudi la kubainisha ukubwa wa tatizo lenyewe kama ugonjwa wa *kansa* ambao hugharimu maisha ya watu wengi kutokana na ukosefu wa tiba yake. Suala la matabaka katika jamii halifai kabisa kwani huigawa jamii kulingana na uwezo walionao, husababisha tabaka lingine kunyanyaswa na kukandamizwa kutokana na uwezo wao kuwa duni. Katika mashairi ya “*Wasakatonge*” (uk 5), “*Mvuja jasho*”, na “*Walala Hoi*” (uk 36) mtunzi anaonesha tabaka la watu wa chini wanafanya kazi kwa bidii sana ili kuweza kujikomboa na kujikwamua na umaskini lakini wanashindwa kufikia matarajio kutokana na malipo duni ukilinganisha na uzito wa kazi wanazofanya na faida wanazopata waliowaajiri. Mfano katika ubeti wa 34 wa shairi la “*Wasakatonge*” kunaelezwa kwamba:

*Wajenga maroshani,
 Waashi kuwa kazini,
 Kwa nyumba zenyе thamani,
 Walalapo huwa hoi,
 Malipo hayalingani,
 Ni walala hoi.*

Katika ubeti huu mtunzi anaonyesha itikadi katika matabaka kwa kubainisha namna kundi la tabaka la juu wanavyofaidi rasilimali za nchi na matunda ya uhuru kwa kuishi kwenye nyumba zenyе thamani na heshima. Wakati huohuo walalahoi ambaario tabaka la chini waliopigani upatikanaji wa uhuru wao hawafaidi matunda hayo kwani kulala kwao ni kwa shida na malipo ya ajira zao hayalingani na uzito wa kazi wanazofanya. Uwepo wa matabaka unajitokeza pia katika mashairi ya “Asali Lipotoja” (uk 37-38), “*Hatuna Kauli*” (uk 8-9) na “*Kosa*” (uk 3).

Utafiti huu unabanisha kuwa suala la matabaka katika jamii ni janga sugulinalokwamisha kufikia ujenzi wa jamii mpya katika Bara la Afrika. Hata hivyo, inaonekana wananchi wameamka na kuanza kudai haki zao kutoka kwa tabaka tawala kupitia katika shairi la “*Hatukubali*” (uk 38). Kwa sasa zipo baadhi ya nchi katika bara la Afrika raia wao wameamua kuingia barabarani kudai haki zao kwa kutumia nguvu ya umma angalia nchi ya Mali, Libya, Misri, Tuniasia na kadhalika. Mawazo ya nadharia ya U-marx yanatufunza kwamba, wananchi wanaponyonywa kwa muda mrefu na tabaka tawala hufikia katika hatua ya kuamua kupigania haki zao bila uoga kwa kuwaondoa madarakani viongozi wanyonyaji na kuwaweka wale ambao ni watetezi wa haki za wanyonge. Wananchi wanapofikia katika hatua hii wanakuwa wameteseka sana na uvumilivu unakuwa umewashinda na hivyo

inajengeka itikadi mionganii mwao kwamba sasa tunapaswa kupambana ili kuwaondoa viongozi hao na hakuna mbadala mwingine wa kukomesha unyonyaji katika jamii yetu.

4.3.6 Itikadi ya Mapenzi

Mapenzi katika kazi za fasihi husawiriwa kwa namna mbalimbali kama vile mapenzi ya mtu na mtu, mapenzi ya mme na mke, mapenzi ya mtu na nchi yake, mapenzi ya mtu na familia yake na mapenzi ya kikundi kimoja na kingine katika jamii (Lyatuu, 2011). Mapenzi ni dhamira inayowasilishwa na watunzi mbalimbali wa kazi za fasihi kama vile, riwaya, tamthiliya na ushairi (Low, 2011). Katika utafiti huu tulibaini kuwa mtunzi katika *Wasakatonge* amewasilisha itikadi ya mapenzi kwa kubainisha kuwa nguvu ya mapenzi huwafanya wawili wapendanao, yaani mme na mke kuweza kusahau karaha zote za dunia ikiwa wote wana mapenzi ya dhati kwa kila mmoja wao. Mtunzi anaonyesha kwamba mapenzi ya dhati hunoga na huzaa faraja kubwa mioyonii mwao kama shairi la “*Yeye na Mimi*” (uk 39) linavyosema;

*Yeye akitabasamu, moyo huuosha,
Hunipandisha stimu, na mwili huniregesha,
Hunizidisha na hamu, mbele yake nimekwisha.*

*Yeye anaponishika, mwili huninyong'onyesha,
Huwa ninapumbazika, na akili hunirusha,
Maraha hukamilika, si pungufu yanatosha.*

Katika dondo hili mtunzi anaonesha itikadi ya mapenzi ni kupendana baina ya mume na mke na kikubwa katika mapenzi ni kutabasamu. Mmoja kati ya wapenzi anapotabasamu maana yake ni kwamba ameridhika na mapenzi anayopewa na

mwenzake na hivyo mapenzi hayo hudumu milele na milele. Hali hii huwafanya wapenzi kuwa kitu kimoja na hakuna kati ya wapenzi ambaye anakuwa ni daraja la juu na mwingine daraja la chini. Tukirejelea mawazo ya nadharia ya U-marx, dondoo hili linarejelea mahusiano baina ya nchi moja na nyingine ambapo nchi hizo zinaposaidiana katika shida na raha zinakuwa kitu kimoja. Kwa maneno mengine mapenzi ya kweli huonekana pale ambapo hakuna unyonyaji baina ya wapenzi au watu wanaopendana.

Itikadi ya mapenzi ya dhati inapatikana katika mashairi mengine kama: “*Nilichelewa Kupendwa*” (uk 41), “*Nilikesha*” (uk 23-24), “*Sitakujua*” (uk 28) “*Usiku wa Kiza*” (uk 27). Tuone mfano kutoka katika shairi la “*Nilikesha*” anasema kuwa:

Nilikesha,
Kuisubiri yetu miadi,
Uwe usiku wa kufaidi,
Kwa kuitekeleza ahadi,
Nikakusubiri kwa hamu,
Kwa shauku na tabasamu,
Nilikesha.

Nilikesha,
Na kulikucha sikukuona,
Nathibitisha wako uungwana,
Kosa langu kukupenda sana,
Hustahiki heshima hiyo,
Sisahau sikusamehe,
Nilikesha.

Dondoo hili linaonesha kwamba mapenzi ya kweli hutawaliwa au hupambwa na uaminifu baina ya wale wanaopendana. Inapotokea mmoja kati ya wapenzi

hatekelezi ahadi kama inavyotakiwa basi hufanya mapenzi kuwa katika hatihati ya kuvunjika kwani mmoja wa wapenzi huona kadharuliwa na hivyo kuamua kuachana na mpenzi wake. Itikadi hii inaweza pia kutazamwa kwa mawanda mapana kwa kutumia nadharia ya U-marx kwamba hatika mahusiano ya kiuchumi baina ya nchi na nchi hudumu zaidi pale kila upande unapotimiza wajibu wake. Ikiwa upande mmoja hautimizi wajibu wake basi inakuwa ni kama upande mmoja ni tabaka la chini na huo usiotekeleza ahadi ni tabaka la juu. Hali hii husababisha mahusiano kuvunjika na wakati mwagine kutokea mifarakano ya mara kwa mara. Mashairi mengine yanayositisitiza itikadi ya mapenzi ya dhati ni “*Kauli Yako*” (uk 27), “*Nilinde*” (uk 15) na “*Tutabaki Wawili*” (uk 26).

4.3.7 Itikadi ya Kufanya Kazi kwa Bidii

Khalifan (2013) anasema kwamba, Kandoro (1972) katika diwani ya *Mashairi ya Saadan* anaonyesha kuwa, ana ari kubwa ya kuhakikisha wananchi wote wanapata maendeleo na wanakuwa na maisha mazuri. Maendeleo haya yatapatikana iwapo tu kila mwananchi atafanya kazi kwa juhudhi na maarifa tena wa kujituma kikamilifu.

Katika utafiti huu mtunzi ameonyesha itikadi ya kufanya kazi kwa bidii kwa kubainisha kuwa baada ya uhuru kupatikana katika nchi nyingi za Bara la Afrika watunzi mbalimbali waliandika mashairi kwa lengo la kuhamasisha na kuhimiza ujenzi wa jamii mpya yenye kuzingatia msingi ya usawa na haki ili kujiletea maendeleo endelevu. Mohammed Seif Khatib kwenye diwani ya *Wasakatonge* katika shairi la “*Klabu*” (uk 50) Ubeti wa 9 na 10 mtunzi anasema:

*Tusiwe tegemezi,
Ila tuchape kazi,*

Tutumiye ujuzi.

*Tuvijenge viwanda,
Na kilimo kutanda,
Ufugaji kushinda.*

Itikadi ya kufanya kazi kwa bidii na maarifa inawasilishwa vema katika dondoo hapo juu ambapo wananchi wanahimizwa kujitegemea kwa kufanyakazi kwa kutumia ujuzi na maarifa. Itikadi hapa ni kwamba, kufanya kazi bila maarifa ni hatari sana kwani hakuna tija ambayo inaweza kupatikana. Pia, katika dondoo hili kunahimizwa watu kujenga viwanda, kukuza kilimo, na kuimarisha ufugaji ili kufunguwa fursa ya ajira kwa wananchi wakiwemo vijana. Mawazo ya nadharia ya U-marx yanasisitiza wanajamii kujitegemea hasa kwa watu wa tabaka la chini kufanya kazi kwa maarifa ili kukuza mitaji na kuweza kuwa na shughuli zao za uzalishaji mali kwa lengo la kuepuka unyonyaji unaofanywa na tabaka tawala. Itikadi ya kufanya kazi kwa juhudii na maarifa husaidia kukuza utu na heshima katika jamii.

4.3.8 Itikadi ya Maadili na Malezi

Zipo baadhi ya jamii ambazo huamini kwamba ili mtoto awe na maadili ni lazima alelewe na wazazi wote wawili, (Lyatuu, 2011). Ikiwa mtoto amealelewa na mzazi mmoja na mzazi huyo akawa ni mama basi watu wengi huamini kuwa mtoto huyo hawezni kuwa na maadili. Hata hivyo, hii ni itikadi tu kwani wapo baadhi ya watoto wa kike wamelelewa na wazazi wote wawili lakini hawana maadili na wapo ambao wamelelewa na mama tu lakini wana maadili na heshima kwa watu wote katika jamii.

Utafiti huu unabainisha itikadi ya mtunzi kwa kuonyesha namna mmomonyoko wa maadili katika jamii ilivyoshika kasi kubwa kutokana na ukuaji wa maendeleo ya sayansi na teknolojia ambayo imesababisha jamii kukosa mwelekeo uliokuwa mwema. Katika shairi la “*Jiwe si Mchi*” (uk 18) ubeti wa 1 na 2 mtunzi anasema kuwa:

Vinu wenzake ni michi, wala sibadilishe,
Ufundi haujifichi, utwanzi na mizunguwe,
Jiwe la manga si fichi, haitakidhi hajawe,

Nafaka haziwi unga, kwa kusagiwa na jiwe,
Utaambulia chenga, mapishi yakuumbuwe,
Ni lazima kuzitwanga, kinuni zishindiliwe.

Katika beti hizi mtunzi amegusia mambo ambayo yanaenda kinyume na maadili na malezi ya Kiafrika kwani ameonyesha jinsi wanawake Wakiafrika wanavyokutana kimwili wenyewe kwa wenyewe jinsia moja (wasagaji). Jambo hili siyo itikadi za nchi za Kiafrika na mtunzi wetu ameonyesha namna jamii zetu zinavyopokea itikadi za jamii za nje na kuiga bila kujali athari zake katika maadili ya jamii zao.

Mohammed Seif Khatib anaiasa jamii kuachana na itikadi za nje unaosababishwa na kuheshimu mila na desturi zetu zinazozingatia msingi wa dini wa mme na mke katika ndoa. Kimsingi, mawazo ya nadharia ya U-marx yanaeleza kwamba ni kawaida kwa binadamu kuiga mambo au utamaduni wa tabaka ambalo linaonekana ni la juu na kwa muktadha huu mataifa ambayo yameendelea. Haya hivyo, si kila jambo ambalo linafanywa na watu wa mataifa yaliyoendelea ni zuri kwa kila jamii. Nadharia ya U-marx inaitaka jamii kujikita katika katika misingi yake ya maadili ili kuweza kufikia

maendeleo ya kweli ya uchumi, siasa, kijamii na kiutamaduni. Jamii inapokengeuka na kuanza kuiga na kufuata mila na desturi za jamii nyingi hasa zile ambazo haziendani na utamaduni wa jamii husika basi hapo kutakuwa na tatizo katika kufikia maendeleo ya kweli.

4.2.9 Itikadi ya Uchu wa Madaraka na Uongozi

Itikadi ya uchu wa madaraka na uongozi ni mionganini mwa itikadi zinazojitokeza katika diwani ya *Wasakatonge*. Suala la uchú wa madaraka hujitokeza zaidi pale baadhi ya viongozi wanapomaliza muda wao wa uongozi wanakataa kutoa madarakani ili kupisha wengine waingie. Hali hii husababisha machafuko na baadhi ya nchi kuingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Shairi la “*Tonge la Ugali*” katika ubeti wa 4 mshairi inaeleza:

Wanapigana,
Waumizana,
Wanauwana,
Kwa tonge la ugali!

Tonge la ugali hapa ni msimbo wa kiishara ambao unaashiria utamu wa madaraka ambao huwafanya baadhi ya viongozi kukataa kutoka madarakani. Viongozi hao wapo tayari kupigana na kuuwana kwa sababu tu ya kuendelea kudumu katika madaraka. Nadharia ya U-marx inaeleza kwamba tabaka tawala siku zote lipo kwa ajili ya kunyonya wananchi wa tabaka la chini. Unyonyaji unapokomaa inakuwa ni itikadi kwamba hakuna kutoka madarakani ili kuendelea kuinyonya jamii. Si jambo jepesi kwa binadamu wengi kukubali kuachia madaraka kirahisi ila pale panapokuwa na misingi mizuri ya demokrasia ndipo inakuwa ni rahisi kwa viongozi waliopo madarakani kukubali kuondoka pale muda wao unapofika.

4.3.10 Itikadi ya Unafiki na Usaliti katika Jamii

TUKI (2004) inaeleza kwamba usaliti ni tendo la kutoa siri za mtu, kikundi, au nchi kwa adui wa mtu, kikundi au nchi hiyo. Katika jamii wapo watu ambao kazi yao ni kufanya fitina na usaliti katika maisha yao ya kila siku na huona fahari kutekeleza azma zao. Usaliti na fitina hufanywa kwa lengo la kupata maslahi kwa mfitini pale aliowarfati wanapokosana na kupigana. Tumeona baadhi ya wananchi wamefanyiwa fitina ya kugombanishwa na serikali yao na kisha kufanikiwa kuiondoa serikali madarakani na leo wanapata taabu ya maisha magumu. Wale ambao walifanya fitina hiyo, wao sasa hivi wananaufaika na rasilimali za nchi hiyo. Katika shairi la “Vinyoga” na “Waramba Nyayo”. Mfano mtunzi katika shairi la “Waramba Nyayo” ubeti wa 3, 4 na 5 anasema kuwa: -

*Wajikweza kwayo,
Bila na hata nadharia,
Kusudiyo.*

*Wajikomba,
Ili kuvipata vyeo,
Na uluwa.*

*Wanawaponza,
Kuwataliti wenzao,
Hawajali.*

Dondoo hili linathibitisha kwamba mara nyingi itikadi ya fitina hujengwa na kutamani vyeo ili kupata maslahi makubwa na wale ambao wanafanyiwa fitina kuwa na maisha mabaya. Fitina hufanywa kwa namna nyingi sana na mtunzi anaeleza kwamba wapo baadhi ya watu hufanya fitina na usaliti kwa kujikomba kwa viongozi

na kuwaeleza maneno ya uongo dhidi ya wengine. Dondoo linaendelea kuonesha kwamba, mtu mwenye itikadi ya fitina na usaliti kama njia ya yeye kufanikiwa huwa hajali madhara yanayoweza kumpata yule aliyemfitini na kumsaliti. Mawazo ya nadharia ya U-marx yanasisitiza umuhimu wa kila mwanajamii kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa ili kupata kipato halali cha kujikimu na kisha kutokuwa na haja ya kuwafitini wengine ili kupata kipato.

4.2.10 Itikadi ya Dini

Dini inaelezwa kuwa ni imani ya kumuamini na kumtii Mungu wa haki (TUKI, 2004). Dini ni asasi mojawapo ya kiutawala ambayo huweza kutumiwa kuwapumbaza wanyonye wasione ukweli (Marx & Angels, 1948). Wataalamu hawa wanaendelea kueleza kwamba, dini hutumiwa kueneza itikadi za uongo za tabaka tawala ili liendelee kuthibiti mamlaka ya utawala na nguvu za kiuchumi. Hufanya hivi kwa kueneza dhana ya majaliwa kumaanisha kuwa Mungu ameratibu maisha ya wanadamu na yote wanayoyapitia ni mpango wa Mungu. Hii inamaanisha kuwa kama jamii ni maskini basi ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu wawe hivyo.

Itikadi ya dini inajitokeza katika mashairi ya *Wasakatonge* kupitia mashairi ya, “*Waso Dhambi*”, “*Vinyonga*”, “*Uasi*” na “*Pepo Bila Kifo*”. Katika shairi la “*Uasi*” kwa mfano kwenye ubeti 2 na 3 katika shairi la “*Wasio Dhambi*” mtunzi anasema kwamba:

Wavilemba!
Wavilemba, na majoho, tasibini,
Wajigamba, safi roho, ni kebehi,
Wanotenda,
Unafiki.

Warozari!

Misalaba, na majuba, na hotuba,

Nyingi toba, zeny'e hiba, na haiba,

Mambo yao,

Unafiki.

Katika dondo hili inaonyesha kwamba, wapo baadhi ya watu ambao wana itikadi ya dini lakini wanatumia dini vibaya. Lengo la dini ni kumfanya mwanadamu kuwa mtu mwema ambaye ataishi maisha yake kwa kuwajali na kuwatendea mema watu wote. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo kumeripotiwa viongozi wa dini wakijihuisha na vitendo viovu kama ubakaji na ulawiti mambo ambayo ni kinyume kabisa na maadili na mafundisho ya dini. Watu wa aina hii wanatajwa kuwa ni wanafiki na itikadi ya dini waliyonayo ni kwa ajili ya unyonyaji kwa watu wengine.

Si hivyo tu, bali pia katika jamii wapo baadhi ya watu ambao hujifanya ni washika dini sana lakini ni wezi wa mali za waumini wao kwa ajili ya maendeleo binafsi. Hili mi jambo ambalo lipo kinyume na maadili na mafundisho ya dini. Ndio maana katika mafundisho ya nadharia ya U-marx wao wanasema kwamba, dini ni chombo cha unyonyaji ambacho kinatumiwa na baadhi ya watu hasa viongozi wa dini katika kujinufaisha wao binafsi kwa kuwaibia waumini wao. Dini ni chombo cha kuwapumbaza watu ili wanaponyonywa na kuibiwa mali zao wasihoji. Haya ndiyo mawazo ya wana nadharia ya U-marx ambayo yanaonekana kuwa na ukweli fulani. Hata hivyo, katika hali halisi dini ni chombo kizuri ambacho huwafanya wanadamu kuwa wanyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na kuwatendea wema wanadamu wenzao. Kutumika vibaya kwa dini kusiwe ni sababu ya kuiona dini kama kitukibaya bali wabaya ni watu wachache ambao wanaitumia dini vibaya. Haya

yanajibainisha pia katika shairi la “*Vinyonga*”. Mfano katika ubeti wa 3 mtunzi anasema kuwa:

Membari,
Imevamiwa,
Na waumini vinyonga,
Wakiwa juu ya viriri,
Hayo wanayohubiri,
Na wanayo yakariri,
Syo hasa wayatendayo,
Ni dhambi tupu.

Kimsingi, dondo hili linashadadia kile ambacho kimeelezwa hapo juu kwamba wapo baadhi ya waumini wa dini hutenda mambo tofauti na yale ambayo wanahubiri au kuhubiriwa wanapokuwa katika nyumba za ibada. Jambo hilo halikubaliki na ni kinyume na maadili na mafundisho ya dini.

4.3.11 Itikadi ya Kimapinduzi

Katika utafiti huu, mtunzi wetu ameonyesha itikadi ya kimapinduzi kwa kuonyesha namna anavyojali jamii yake kwa kubainisha matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii yake bila kuogopa watawala katika nchi. Katika bara la Afrika hususani Tanzania mtunzi amebainisha changamoto zinazokabili jamii na kuonesha namna ya kuzitatu ili kuweza kufikia ujenzi wa jamii mpya. Matatizo hayo ni kama vile, unyonyaji, dhuluma, uongozi mbaya, ugandamizaji, uonevu, matabaka, unafiki na usaliti. Mfano katika shairi la “*Wasakatonge*” na shairi la “*Afrika*” katika ubeti anasema kuwa:

*Jua kali na wasakatonge
 Wao ni manamba mashambani,
 Ni wachapa kazi viwandani,
 Mayaya na madobi wa nyumbani,
 Ni matopasi wa majaani,
 Lakini bado ni maskini.*

Katika dondo hili kunasawiriwa hali halisi ya maisha ya watu wanyonge katika jamii, ambao hujituma katika kufanya kazi lakini hawapati faida yoyote kutokana na kujituma kwao. Sababu kubwa ya hali hii ni unyonyaji ambao umekithiri katika jamii na hivyo ili kuepukana na hali hii basi vijana wanapaswa kujitambua na kudai haki zao. Kwa mujibu wa nadharia ya Umarx inaelezwa kwamba tabaka tawala hunonya rasilimali na nguvu kazi ya tabaka tawaliwa na kuliacha tabaka hilo katika umasikini. Njia muafaka ya kumaliza tatizo hilo ni kufanya mapinduzi ya kifikira ili kujitambua na kuondokana na unyonyaji unaosababisha na kuendeleza umasikini katika jamii.

4.3.12 Itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea

Nyerere (1968, 1977) anasema kwamba, ujamaa umelenga katika kuleta usawa wa binadamu katika nyanja mbalimbali za maisha, na kuongeza kuwa ujamaa na uhuru ndio nguzo kuu za ujenzi wa jamii mpya ya kijamaa. Katika utafiti huu, mtunzi anaonyesha kuwa ni muumini wa sera za ujamaa na kujitegemea kwani ameonesha namna jamii inavyopita katika wakati mgumu sana kwa sababu ya kukosa usawa, umoja na mshikamano katika masuala ya kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kifikira. Mtunzi anasema kuwa, uhuru ni njia mojawapo ya kujitoa katika utawala wa kikoloni. Katika shairi la “*Nuru ya Tumaini*” mtunzi wetu anasema kwamba:

*Wingi linatoweka,
Lililowagubika,
Mia tatu miaka,
Wana wa Waafrika,
Wamedharaaulika,
Hatima mefikiya.*

*Wafutwa ubaguzi,
Ule wa walowezi,
Wa nasaba na ngozi,
Mabwana na washenzi,
Ni vya uangamizi,
Mwisho wake mefika.*

Mtunzi anasema kuwa msingi wa ujenzi wa jamii mpya ni kujenga usawa, umoja na mshikamano katika jamii husika ili sera ya ujamaa na kujitegemea iweze kufikiwa kwa lengo la kuepuka ubaguzi wa rangi, matabaka katika jamii, ugandamizaji na unyonyaji. Msitari wa mwisho katika ubeti wa mwisho unasema “mwisho wake umefika,” ikiwa ni kurejelea ujamaa na kujitegemea kama njia muafaka ya kumaliza unyonyaji unaofanywa na baadhi ya watu katika jamii. Ujamaa na kujitegemea ni será ambayo ililenga kuimarisha usawa na ustawi wa watu wote katika jamii na hivyo hakuna mtu ambaye anaweza kumnyonya mtu mwingine kwa sababu wote wanaisha pamoja. Umax unasisitiza sana katika misingi ya umiliki sawa wa rasilimali ili wananchi wote wawewe kufurahia neema zitokanazo na rasilimali hizo na si watu wachache tu katika jamii.

Kimsingi katika sehemu hii mtafiti amefanikiwa kubainisha masuala ya itikadi zinazojitokeza katika kama kupiga vita uongozi mbaya, kuwa na demokrasia ya

kweli na utu, kupinga ukoloni mamboleo, matabaka katika jamii, unafiki na usaliti katika jamii, kufanya kazi kwa bidii, mmomonyoko wa maadili katika jamii, hali ngumu ya maisha, ukombozi wa kisiasa, kiutamaduni, kiuchumi na kifikira/mawazo kutaja kwa muhtasari. Kwa jumla, inaonekana kwamba, mshairi Mohammed Seif Khatibu ni muumini wa mageuzi katika jamii akilenga jamii yenyе usawa na haki isiyokuwa na dhuluma mionganoni mwa wanajamii wake.

4.4 Mbinu za Kisanaa katika Mashairi ya Wasakatonge

Katika sehemu hii tumefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data zinazohusiana na mbinu za kisanaa zilizotumika katika kujenga itikadi mbalimbali katika mashairi ya Mohammed Seif Khatib katika Diwani teule. Mbinu za kisanaa katika kazi ya fasihi ni uwanja mpana mno ambao hatutaweza kuogelea na kumaliza uwanja wote hivyo basi, katika utafiti huu tumeshughulikia tu kipengele kimoja cha mbinu za kisanaa ambacho ni tamathali za usemi. Kipengele cha tamathali za usemi ni kimojawapo kati ya vipengele kadha wa kadha vya matumizi ya lugha. Vipengele vya tamathali za usemi tulivyoshughulikia ni tashbiha, kejeli, takrir, sitiari na misemo.

4.4.1 Sitiari

Mulokozi (1996) anasema kwamba, sitiari ni tamathali ya usemi inayotumika kitu kimoja kuwakilisha kitu kingine ambacho hakina uhusiano nacho. Kwa mfano, baadhi ya washairi wa kiume huwahusisha wapenzi wao wa Kike na “*Ua*” hivyo mshairi, anaposema” “*Ua langu ni zuri* huwa anamsifia mpenzi wake. Sitiari ni uhamishaji wa maana kutoka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Katika utafiti huu, mtafiti amebaini kuwa sitiari imejitokeza katika shairi la “*Tiba Isotibu*” ambamo mwandishi amatumia sitiari “*Ndwele ni Umaskini*” akilinganisha

“Umaskini na Maradhi au Ugonjwa”. Mtunzi anabainisha kuwa katika nchi nyingi za bara la Afrika hususani Tanzania linashindwa kujitegemea kwa kusimamia raslimali zake na hivyo kuwa maskini kutokana na ujinga walionao watu wake. Hivyo basi ili bara la Afrika hususani Tanzania ni sharti kujikomboa kielimu ili wajinasuwe kutoka mikononi mwa wakoloni na kujitegemea katika nyanja zote za maisha. Katika ubeti wa nne wa shairi hilo hilo mtunzi anasema kuwa:

Asema,
Ndwele ni umasikini,
Ujinga upo pomoni,
Maradhi yaso kifani,
Bara lilo ujinga,
Lazima tiba.

Inaendelea kusisitizwa kwamba adui ujinga ni mbaya sana na anaweza kuondolewa kwa kupatiwa tiba ambayo ni elimu. Tiba hiyo ya elimu itasaidia pia kutibu adui wengine wawili amba ni maradhi na umasikini. Hapa tunaona matumizi ya msimbo wa kiishara wa nadharia ya Simiotiki ukijitokeza bayana ambapo elimu inatajwa kwa ishara kama ndiyo tiba na suluhisho na matatizo ambayo yanalikumba bara la Afrika.

4.4.2 Tashibiha

Senkoro (1982) anasema kwamba, tashibiha ni tamathali ya usemi ambapo watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa na watu ama vitu vingine kwa kutumia maneno kama; mithili, kama kwamba, kama vile, mfano wa, na mengine ya aina hiyo. Tashibiha ni tamathali ya ulinganisho kwa kitu kimoja kulinganishwa na kingine kwa sifa au tabia (Mulokozi, 1996). Katika diwani ya *Wasakatonge* kuna matumizi ya tashibiha katika mashairi mbalimbali kwa mfano shairi la “*Kansa*” mtunzi anasema kuwa:

*Imekuwa ni donda, donda lisotibika,
Limeanza kuvunda, kuvunda kupasuka,
Lanuka kama ng'onda, ng'onda asokauka.*

*Kwenu natoa wito, wito kuelekeza,
Dawa yake si nzito, nzito kutekeleza,
Msumari wa moto, moto ni kuingiza.*

Katika ubeti hizi mbili tashibiha inajitokeza katika misitari isemayo, *Lanuka kama ng'onda* na *Msumari wa moto*. Tukirejelea msimbo wa kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki tunaona hapa msanii akiifafanua itikadi ya utegemezi kama kitu kibaya sana ambacho huitafuna jamii na taifa kama ilivyo kwa kidondo cha kansa kisichotibiwa ambacho bila shaka humshambulia binadamu hata kumfanya kupoteza uhai wake. Dawa ya kuondoa utegemezi kutoka kwa wageni ni hiyo inayotajwa ya kupata msumari wa moto na kuchoma kidonda hicho. Hii kwa mujibu wa msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki ina maana kwamba kuondoa utegemezi kwa kujitegemea ndiyo itikadi muafaka ambayo itaziwezesha nchi za Afrika kutweza kutumia vizuri rasilimali zao na kuwanufaisha wananchi wa nchi zake.

4.4.3 Takriri

Takriri ni tamathali ya semi inayobainisha kitendo cha msanii kuruduarudia maneno, sauti, wazo au jambo fulani katika kazi yake ya fasihi. Aina tafauti za urudiaji tunaweza kuwa na aina mbalimbali za takriri kama vile takriri wazo, takriri mistari, takriri wazo, takriri irabu, takriri konsanati na kadhalika. Watunzi katika kazi ya fasihi hutumia takriri ili kutia msisitizo wa jambo fulani kwa kuwafanya wananchi kujithari na kutafuta kinga kwa jambo lenyewe ili kuepuka mathara yanaweza

kujitokeza kwa jamii husika. Mtunzi ametumia neno *Jamii imeoza imeonza ya nuka* neno “Oza” hapa mtunzi anasisitiza kuwa jamii ipo katika kipindi kigumu kwani katika bara la Afrika kumejaa kila aina ya uchafu na uozo wa kila aina kwani ubaya, ugandamizaji, unyonyaji, uonevu, fitina njaa, umaskini na magonjwa imekuwa ndio maisha ya kila siku katika jamii na viongozi wao wanatumia madaraka yao kujinufaisha wao wenyewe na familia zao mfano katika shairi la “Afrika” mtunzi anasema kuwa:

Lini?

Afrika utakuwa,

Bustani ya amani,

Ukabila kuuzika,

Udini kuufyeka,

Ni lini?

Lini?

Afrika utakuwa,

Ziwa la utulivu,

Kufisha uonevu,

Kumaliza uovu,

Ni lini?

Katika dondoo hili tunaona matumizi ya takriri ni “lini” ambayo katika kila ubeti imejitokeza mara mbili. Ujitokezaji wake unafanyika mara mbili ikiwa ni mwanzoni na mwishoni mwa ubeti kama msisitizo kwamba nchi za Afrika zinapaswa kufanya jitihada ili kujikombua katika nyanja zote za maisha. Msimbo wa Kihemenitiki wa nadharia ya Simiotiki unatusaidia kuelewa kwamba, itikadi ya ukombozi hasa wa kiuchumi inatakiwa kufanya mapema na kwa kutumia jitihada nyingi za ushirikiano baina ya mataifa ya Afrika.

4.4.4 Ishara

Wamitila (2008) anasema kwamba, ishara ni mojawapo ya matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi ambayo hutumika kutoa ishara juu ya jambo au dhamira fulani ambayo mwandishi anataka hadhira yake ipate au ifahamu. Matumizi ya ishara yanajitokeza katika shairi la *Tonge la Ugali* (uk.20) mtunzi anasema kuwa:

Wanasemana,
Wanasutana,
Wanakanyana,
Kwa tongue la ugali!
Wasengenyanana,
Wazomeana,
Wanang'ong'ana,
Kwa tongue la ugali!

Katika dondo hili “tonge la ugali” limetumika kama ishara ya rasilimali za taifa ambazo watu wachache huzitumia kwa masilahi yao binafsi na si kwa masilahi mapana ya jamii nzima. Tunaporejelea msimbo wa Kiishara wa nadharia ya Simiotiki tunapata kufahamu kwamba, ugali ni chakula ambacho kinaliwa na jamii nyingi za nchi ya Tanzania, Afrika na sehemu mbalimbali ulimwenguni. Hivyo ni chakula kinachopendwa na watu wengi ambayo sasa ni ishara ya namna baadhi ya watu wachache wanavyopenda kujinufaisha wao wenyewe kwa rasilimali za taifa na kuwadhulumu wanajamii wengine. Itikadi ya upendo na kuthamini watu wengine katika jamii ni jambo ambalo linapaswa kujengwa na kuenziwa katika jamii.

4.4.5 Picha na Taswira

Alhabib (2022) anasema kwamba, katika diwani ya *Wasaka Tonge* mtunzi anazungumzia masuala ya fani, kwani ameonyesha umahiri wa kisanii. Mashairi

yenye mvuto kisanaa yameshibishwa si katika maudhui tu, bali hata katika fani. Matumizi ya picha ni moja kati ya tamathali za semi zilizotumika katika *Wasakatonge* na hapa tuone mfano wa shairi la “*Buzi lisilochunika*” mtunzi anasema kuwa:

*Hili buzi buzi gani, buzi lisilochunika,
Halina ngozi laini, inayoweza kutoka,
Lina manyoya mwilini, ambayo yamefunika.
Msumeno utafute, na makali kuyaweka,
Ukwereze na uvute, na watu kukusanyika,
Na hutafika popote, buzi halitachunika,*

Kiitikio

*Hili buzi gani, buzi lisilochunika,
Ngozi yake si laini, ngumu isiyobanduka.*

Mtunzi katika mashairi hayo amewasilisha ujumbe wake kwa ukali sana jambo ambalo angetumia lugha ya kawaida katika kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii husika hakika jamii ingemuona mtunzi kama anatumia lugha ya matusi na lugha isiyofaa kwa jamii yake. Tukirejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kimatukio tunaona matumizi ya lugha ya picha yakijitokeza katika dondoo kumaanisha umuhimu wa itikadi ya kujitegemea katika jamii. Suala la kutegemea misaada kutoka kwa mtu au taifa fulani ni jambo ambalo halina uhakika na mwendelezo yaani, si jambo la kudumu. Hivyo, kujitegemea ndiyo msingi wa maendeleo katika jamii.

4.5 Hitimisho

Sura hii imefanikiwa kuwasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti kwa mujibu wa malengo mahususi mawili ya utafiti huu. Kwanza tumewasilisha kuhusu itikadi

mbalimbali zinazojitokeza katika diwani ya Wasakatonge na kisha tumewasilisha mbinu za kisanaa za tamadhali za semi ambazo zimetumika katika kujenga dhamira ya itikadi katika diwani teule. Kwa jumla, tumeona itikadi mbalimbali na hapa tumetaja kwa uchache itikadi kama kupiga vita uongozi mbaya, uwepo wa matabaka, itikadi ya kimapinduzi, itikadi ya mapenzi, itikadi ya ujumaa na kujitegemea, itikadi ya Dini, itikadi ya maadili na malezi, itikadi ya unafiki na usaliti katika jamii na itikadi ya kufanya kazi kwa bidii. Kuhusu mbinu za kisanaa tumewasilisha vipengele vya sitiari, tashibiba, takrir, ishara na picha. Mbinu hizi za kisanaa zimesaidia kujenga dhamira ya itikadi katika diwani teule. Sura inayofuata inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ndiyo sura ya mwisho katika tasinifu hii ambayo lengo lake ni kutoa muhtasari, hitimisho na mapendendekezo. Katika kutekeleza lengo hili, sura hii imeandikwa kwa kuzingatia malengo mahususi mawili ya utafiti ambapo lengo la kwanza lilikuwa ni kubainisha itikadi zinazojitokeza katika mashairi ya diwani ya Wasakatonge na lengo mahususi la pili lilikuwa ni kuchambua mbinu za kisanaa za tamathali za semi ambazo zimetumika katika kujenga itikadi katika diwani ya *Wasakatonge*.

5.2 Muhtasari

Kwa upande wa itikadi zilizojitokeza katika diwani teule tumeweza kuwasilisha kadhaa lakini hapa kwenye muhtasari tutazungumzia chache tu ambazo ni kupiga vita uongozi mbaya, demokrasia na utu wa kweli, ukoloni mambo leo, matabaka na kufanya kazi kwa bidii. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba jamii ina itikadi kwamba uongozi mbaya ni adui mkubwa wa maendeleo yao na hivyo ni vema kupamabana na adui huyo ili kuhakikisha maisha ya wanajamii wote yanakuwa mazuri. Haya yameonekana kupitia shairi la *Dikteta* (uk.21) na shairi la *Nahodha* (uk.41). Jamii inapokuwa na uongozi mzuri ni rahisi sana kupata maendeleo kwa haraka kuliko kuwa na uongozi ambao unafanya kazi kwa masilahi binafsi na maslahi ya watu wachache. Hii ni itikadi endelevu kwani katika jamii zetu viongozi wabinafsi hawakosekani na kila mara tumeona wananchi wakilalamika na viongozi wa ngazi za juu wakichukuwa hatua za kuwaondoa katika uongozi wanaolalamikiwa.

Suala la demokrasia ya kweli na utu nalo pia ni moja kati ya itikadi ambazo zimekuwa zikipigiwa kelele na wananchi na jumuiya za kikanda na kimataifa wakitaka wananchi wawe na demokrasia ya kufanya mambo yao ikiwa ni pamoja na kuchagua viongozi. Suala hili tumeliona katika mashairi ya *Saddam Hussein* (uk.26-27) na *Unyama* (uk.47-48). Itikadi ya demokrasia ya kweli na utu husaidia katika kukuza na kuimarisha amani na utangamano katika jamii. Mahali ambapo demokrasia inaminywa huwa kunakukwa na machafuko na amani kukosekana. Tanzania ni mionganini mwa nchi za Afrika ambazo zinaheshimu na kusimamia demokrasia ya kweli na utu mpaka kuitwa kuwa ni kisiwa cha amani ambapo nchi nyingi zinaiga mfano wa Tanzania.

Ukoloni mamboleo ni adui mkubwa wa maendeleo ya bara la Afrika na kwingineko duniani. Katika *Wasakatonge*, mshairi anasisitiza itikadi ya kupambana na ukoloni mamboleo ili wananchi wawzeze kunufaika na matunda ya nchi zao. Mashairi kama *Hatua Kali* (uk.8-9) na *Tiba Isiyotibu* (uk.18) yanatoa msisitizo wa kuhakikisha kwamba jamii inapambana kikamilifu kukomesha ukoloni mamboleo na badala yake kuimarisha ujamaa na kujitegemea. Ukoloni mamboleo ni njia nyingine ya kunyonya rasilimali za Afrika kijanja huku wakoloni walewale wakiendelea kunifaika na utajiri wa mataifa masikini na wananchi wakibaki na umasikini uliokithiri. Hatua kali za kujitegemea ziendelee kuchukuliwa ili kuhakikisha mambo yanakuwa vizuri na rasilimali zinawanufaisha wananchi masikini ili waondokane na umasikini. Hii inakwenda sambamba na itikadi ya kupunguza utabaka na kufanya kazi kwa bidii kama ni moja kati ya masuluhisho ya kuondokana na utegemezi kutoka katika mataifa yaliyoendelea. Kufanya kazi kwa bidii kunasisitizwa katika mashairi ya

Klabu (uk.50) na *Wanawake wa Afrika* (uk.2-3). Kuhusu itikadi ya kupunguza utabaka tunaiona katika mashairi ya *Kansa* (uk.4), *Wasakatonge* (uk.5) na *Walalahoi* (uk.36).

Kwa upande wa mbinu za kisanaa ambazo zimetumika katika kujenga itikadi katika diwani ya Wasakatonge ni pamoja na tamathali za semi za sitiari, tashibiha, takriri, ishara na picha. Kupitia mbinu hizi mtunzi ameweza kuisanifu vizuri dhamira ya itikadi katika diwani teule na kutuwezesha sisi kupata data za utafiti. Kwa jumla, msanii ni bingwa sana wa matumizi ya lugha na hususani lugha ya tanathali za semi ambazo ndani yake mna utajiri mkubwa wa dhamira ikiwemo kuhusu itikadi mbalimbali ambazo tumezibainisha katika matokeo ya utafiti huu. Tamthali za semi ni mbinu muafaka katika ushairi kwa sababu zinawezesha kutumia maneno au maelezo machache kueleza mambo mengi kwa wakati mmoja.

5.3 Hitimisho

Kwa jumla, matokeo ya utafiti huu yamebaini kwamba diwani ya *Wasakatonge* imesheheni dhamira ya itikadi iliyojengwa kupitia mbinu mbalimbali za tamathali za semi. Itikadi kuu inaonekana kuwa ni ukombozi wa jamii hasa kifikira na kiuchumi kwani kwa ilivyo hivi sasa nchi nyingi za Afrika na Tanzania ikiwemo zipo katika hatua nzuri za kuhakisha rasilimali za nchi zinawanufaisha wananchi na si wageni. Tumeona katika suala la mikataba ambapo sasa katika mikataba ya madini Tanzania kwa mfano inapata asilimia 50 na mwekezaji pia anapata asilimia 50 ya faida inayotokana na uwekezaji. Hii ni hatua nzuri sana ya kiukombozi ambapo ukoloni mamboleo hautakuwa na nafasi katika jamii ya Watanzania n anchi mbalimbali pia duniani hasa katika mataifa yanayoendelea. Nchi zilizoendelea zimekuwa zikifanya

ujanja wa kutoa misaada ya aina mbalimbali kwa nchi masikini lakini ukweli ni kwamba misaada hiyo ni kitu kidogo tu ikilinganishwa na faida kubwa wanayoichota kutoka katika bara la Afrika na mabara mengine ya nchi za ulimwengu wa tatu. Mashairi ya Wasakatonge si tu kwamba yanaonesha tatizo au matatizo yaliyopo bali pia yanatoa mapendekezo ya kukabiliana na matatizo husika.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Ili kuweza kusaidi kufikiwa kwa haraka ujenzi wa jamii mpya katika utafiti huu, ninatoa mapendekezo ya muhimu ili kusaidia kada mbalimbali za wanataaluma na wasiowanataaluma kujua na kufahamu kuhakiki kazi za fasihi kwa lengo la kusaidia jamii husika.

5.4.1 Mapendekezo kwa Wahakiki

Mtafiti katika utafiti huu inatoa mapendekezo yafuatayo kwa makundi mbalimbali katika kazi za fasihi ili kujenga uwelewa Mkubwa kuhusu masuala ya Itikadi. Mtafiti anawahasa wahakiki wa kazi za fasihi waendelee kutumia taaluma yao kushughulika na ujenzi wa jamii mpya kwa kuhakiki kazi za fasihi kwa mapana zaidi ili kuweza kusaidia jamii husika kuwa na fikra mpya katika itikadi ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kifkira.

Pia wahakiki waendelee kuhakiki kazi za fasihi katika nyanja nyingine za itikadi za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kifkira lengo kusaidia jamii kufikia ujenzi wa jamii mpya.

Pia napendekeza watafiti kazi zote zinahusiana na masuala ya itikadi zinazofanywa na watafiti siweze kuhakiki na kusalishwa vitabu na marejeo mbalimbali ili kuweza

kuwasaidia wasomaji au jamii lengwa kupata fikra mpya kwani itikadi ndio msingi na mwongozo wa mfumo wa maisha ya kila siku ya binadamu. Katika utafiti huu mtafiti anatambua kuwa majukumu ya wahakiki ni kuhakiki kazi za fasihi

5.4.2 Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari

Katika utafiti huu mtafiti anatoa mapendekezo kwa wachapaji wa magazeti na vyombo vya habari kwa ujumla ili tuweze kufikia ujenzi wa jamii mpya ni vema kama wanahabari kutumia kalamu zao kuandika na kutoa taarifa sahihi kwa jamii ili kuweza kujenga jamii inayoamini uhalsia wa mambo na kuepuka kuandika habari zinazoweza kuleta mgongano na kusababisha kupoteza amani katika nchi.

Pia wanahabari wanawajibu wa kuhubiri uzalendo, umoja na mshikamano katika jamii ili kuweza kuondokana na matabaka, uongozi mbaya, uwepo wa mmonyoko wa maadili na malezi katika jamii, kuondokana na ukoloni mamboleo, kudumisha amani ya nchi, kujenga diplomasia kwa nchi zingine.

Halikadhalika, vyombo vya habari viweze kufanya utafiti kwa kina katika kazi zao za kila siku kabla ya kuwasilisha kwa hadhira husika kwani kwa kufanya hivyo itaepusha nchi kuingia kwenye machafuko au migogoro kwani.

5.4.3 Mapendekezo kwa Watunga Mitaala

Pendekezo langu kwa watunga mitaala wajitahidi kujikita katika kusoma na kupitia kazi mbalimba za fasihi hasa za utafiti zinazofanywa na wanafunzi na wataalumu wetu waohitimu katika ngazi mbalimbali za Elimu ya juu kwani kazi hizo zitakua na mchango mkubwa katika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kifikra.

Serikali iweze kuoma umuhimu mkubwa walionao watunga mitaala kwani wao ndio wanatengeneza fikra mpya kwa jamii kwani watunga mitaala wao ndio kiwanda cha kuanda viongozi wanchi na wataalamu mbalimbali katika taifa. Watunga mitaala wakakozea kutunga mitaala bila kuangalia huitaji wa maisha ya kila siku katika nchi hakika Taifa linaweza kupotea kabisa katika malengo yake ya kufikia ujenzi wa jamii mpya kama anavyozungumzia Muhammed Seif Khatib katika zake za fasihi.

5.4.4 Mapendekezo kwa Utafiti wa Baadaye

Pendekezo kwa watafiti kwa baadae waweze kwenda mbali zaidi kwa kufanya uchunguzi katika Masuala ya falsafa katika mashairi ya kiswahili ya Muhammed Seif Khatib katika ujenzi wa jamii mpya. Pia waweze kuchunguza Itikadi na falsafa ya Mashairi ya kiswahili ya Muhammed Seif Khatib kwa kufanya ulinganisho katika utunzi wa mashairi yake. Waweze kuchunguza pia Mtazamo ya mashairi ya kiswahili ya muhammed Seif Khatib kwa ulinganisho wakati akiwa raia wa kawaida na wakati akiwa kiongozi wa serikali.

5.4.5 Mapendekezo kwa Jamii

Jamii iweze kutilia maanani suala zima la ujenzi wa jamii mpya kama alivyozungumza mtunzi wetu Muhammed Seif Khatib kwani kama jamii itaamua kuungana na kutengeneza umoja na mshikamano suala la uongozi mbaya, mmonyonyoko wa maadili na malezi, Ukoloni mamboleo, rushwa, suala la matabaka, ukosefu wa demokrasia na kadhalika zote hasitakuwa na nafasi katika jamii.

Pendekezo kwa jamii hasa wakati wa kuwachagua viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji, vijiji, mitaa, udiwani, Ubunge na Urais waweze kuzingatia vipengele vyote

vinavyoweza kuwa saidia katika kufikia ujenzi wa jamii mpya kama alivyobainmisha
Mtnzi wetu Muhammed Seif Khatib katika utunzi wa kazi zake.

MAREJELEO

- Alhabib, E. A. (2012). “Matumizi ya taswira katika nyimbo za Taarab,” Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Alhabib, E. A. (2022). “Fani na dhamira katika mashairi ya Dhifa na Wasakatonge.” Tasnifu ya shahada ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ambrose, B. M. (2014). “Kuchunguza dhamira za kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert: Mfano wa *Kusadikika* na *Kufikirika*.” Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Aronson, J. (1992). “A Pragmtic view of thematic analysis in the qualitative report” Vol. 2 No. 1. Searched in. http://www.nova.edu/scs/QR/Black_Issues/QR21/aronson.html, on 23/05/2011, 11:00HRS.
- Babie, E. (1999). *The basics of social research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Barthes, R. (1994). *The Semiotic challenge*. Berkely: University of Califonia Press.
- Bell, F. (1977). “Marxist theory, class struggle and the crisis of Capitalism,” in Jesse Schwartz (ed.), *The Subtle Anatomy of Capitalism*. Santa Monica: Goodyear.
- Bryman, A. (2012). *Social research methods* (2nd edition). Oxford: Oxford University Press.
- Cresswell, J. W. (2009). *Research design: qualitative and methods approaches*. Los Angeles: SAGE Publications
- Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert*. TATAKI: Dar es Salaam.

- Eagleton, T. (1977). "Marxism and literary criticism." In the *Journal of Aesthetics and Arts Criticism* 35 (4): 483-484.
- Enon, J. C. (1998). *Education research, statistics and measurement*. Kampala: Makerere University.
- Cohen, L. (2000). *Research methods in education* (5th edition), London.
- Frolora, N. (2003) "Euphrase Kezilahabi: The renewal of Kiswahili poetry." In *Kiswahili vol. 66* Dar: IKR
- Habwe, J. (1999). "Discourse analysis of Swahili political speeches." Unpublished PhD Thesis.
- Hassan, A. M. (2018). "Kuchunguza falsafa ya mapenzi katika diwani ya Mapenzi Bora." Tasinifu ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ismail, J. H. (2012). "Nafasi ya nyimbo za Bongo Fleva katika uelimishaji wa haki katika Jamii." Katika *Mulika*. Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.
- John, L. (2007). "Critical reading: A guide." In <http://www.Brocku.Ca/English/jige/> Criticle reading. Html Accessed, 30th October 2006
- Kandoro, S. A. (1972). *Mashari ya Saadan*. Dar es Salaam: NPL.
- Kezilahabi, E. (1976). "Shaaban Robert mwandishi wa riwaya." Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. (1977). "Mashairi ya Kiswahili" katika Topan, F. M. (Mh), *Uchambuzi wa maandishinya Kiswahili (Kitabu cha Pili)*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kitogo S.A. (2002). "The poets contribution to political develeopment: Case of Saadan Abdul Kandoro." Unpublished M.A Thesis, UDSM.

- Khalifa, M. Y. (2013). “Siasa katiika ushairi wa Saadan kandoro: Mifano kutoka katika mashairi yake.” Tasnifu ya Uzamivu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Khatib, M. S. (2011). “Chanjo, matakwa ya mwanamume katika mwili wa mwanamke.” Tasnifu ya Uzamivu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Kombo, D. K. and Tromp. D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing: An introduction*. Nairobi: Pauliness Publications.
- Kothari, C. R. (2004). *Reseach methodology: Methods and techiniques* New Delhi: New Age International Publishing Ltd.
- Kothari, C. R. (2008). *Research methodology: Methods and techiniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd
- Linebaugh, P. (1976). “Karl Marx, The theft of wood, working class composition: A contribution to the current debate,” in the *Journal of Crime & Social Justice Vol. 6*
- Low, N. R. (2011). “Athari ya lugha katika kuibua dhamira: Mifano kutoka nyimbo za kizazi kipyaa zinazohusu UKIMWI”, Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Loewenstein, R. M. (1953). *Drives, affects and behavior*. London: Internatonal Universities Press.
- Lyatuu, J. (2011). “Usawiri wa wanawake katika fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa kike na kiume: Uchaguzi katika riwaya teule.” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Maitaria J. N. (2012). “Uainishaji wa ushairi wa Kiswahili kwa kutumia kigezo cha methali.” Katika *Mulika*. Dar es Salaam: TUKI.

- Mark, G. (1995). *Postmodern semiotics: Material cultura and the forms of Postmodern Life*. Oxford: Basil Black well.
- Marx, K. (1979). *Pre-Capitalist social economic formation*. Moscow: Progress Publishers.
- Marx, K. & Engels, F. (1977). *The German ideology*. London: Lawrence and Wishart.
- Marx, K. and Angels, F. (1848). “The Communist Manifesto.” In *Marx & Angels Collected Works, Vol. 6, 1845-1848*. New York: International Publishers.
- Mayoka, J. (1983). *Mgogoro wa ushairi na diwani ya Mayoka*. Nairobi: EALB.
- McCloskey, H. J. (1964). “Would any being merit worship? In the *Southern Journal of Philosophy*,” Vol. 2 Issue 4:157-164.
- Mehring, F. (1962). *Karl Marx. The story of his life*. Ann Arbor: University of Michigan Press.
- Mlacha, A. K. S. & Madumula J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP.
- Msuya, M. B. & Lupokela, A. P. (2012). “Dhima ya bongo fleva katika maadili na malezi kwa jamii.” Katika *Mulika*, Dar es Salaam TATAKI.
- M pangala, G. P. (1977). *Political and social development in Afrika*. Dar es Salam: DUP.
- M pangala, G. P. (2004). “Conflict resolution and peace building in Africa as a process: Case studies of Burundi and the Democratic Republic of Congo.” Dar es Salaam: MNF, *Nyerere Week Conference*.
- Mrekwa, A. (2013). “Matumizi ya picha na taswira katika ushairi wa Kaluta Amri Abedi.” Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

- Mulokozi, M.M., (1975), “Revolution and reaction in Swahili poetry”. *In Kiswahili, Vol. 45/2.* Dar es Salaam: IKR, Kur. 46-65.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, TUKI: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. na K. K. Kahigi (1982). *Kunga za ushari na diwani yetu*. Dar es Salaam: DUP.
- Mulokozi, M.M. na T.S.Y. Sengo (1995). *History of Kiswahili poetry [AD 1000-2000]*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nazarova, T. (1996). *Linguistics and literary semiotics*. Moscow: Moscow State University Press.
- Nowottny, W. (1972). *The Language poets use*. London: The Attilone Press.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Island: Augustana College.
- Nyerere, J. K. (1968). *Ujamaa*. Nairobi: Oxford University press.
- Nyerere, J.K. (1977), *The Arusha declaration: Ten years After*, Dar es Salaam: Government Printer.
- Omari S. (2009). *Tanzanian hip hop poetry as popular literature*: Unpublished PhD thesis, UDSM.
- Omary, M. (2011). “Siasa katika ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008).” Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Pella, D. N. (2018). “Matumizi ya picha na taswira katika Mashairi ya Mohammed S. Khatib: Uchunguzi katika diwani za Fungate wa Uhuru (1988) na Wasakatonge (2003). Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Robson, C. (2007). *How to do a research Project: A guide for undergraduate students*. Carton Victoria: Blackwell Publishing.
- Sanka, S. M. (1994). "Semantic deviation in Iraqw oral poetry". Unpublished M.A Dissertation, UDSM.
- Sengo, T. S. Y. M. na Kiango, S. D. (2012). *Hisiya Zetu*, Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya majaribio: Makutano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi", katika *Kioo cha Lugha, Juzuu, I*.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.
- Shemweta, G. (2015). "Itikadi katika tamthiliya za Emmanuel Mbogo: Utafiti linganishi wa Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo." Tasnifu ya Umahiri katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press: Nairobi.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa tamthilia, historia na maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Msingi na vipengele vyake*, Nairobi: Phonix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Fasihi, istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Msingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide – Muwa.
- Wright, W. (1975). *Sixguns and society: A structural study of the Western*. Berkeley: University of California Press.
- Yin, R. K. (2001), *Case study research: Design and methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO NAMBA MOJA: MUONGOZO WA USOMAJI MAKINI

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi katika matini ambapo katika utafiti wetu matini ilikuwa ni diwani ya Wasakatonge. Kwa kuwa ukusanyaji wa data ni kazi ya kitaalamu na kisayansi tulifuata hatua zifuatazo katika kukusanya data za utafuti huu:

Hatua ya kwanza: Kusoma diwani teule mara tatu bila kudondo data ya aina yoyote. Mtafiti katika hatua hii alilenga kuifahamu vizuri diwani husika kabla ya kuanza kukusanya data za utafiti ili kuweza baadae kupata data zinazohitajika katika utafuti.

Hatua ya pili: Kuandaa mada kulingana na malengo mahususi ya utafuti. Katika hatua hii mtafiti aliandaa mada ambazo zilihitaji kupatiwa data kutokana na malengo mahususi ya utafuti wake. Mada hizo ziliandikwa katika shajara maalumu la kukusanya data na kila mada kupatiwa nafasi ya kutosha ya kudondolea data.

Hatua ya Tatu: Kudondo data kutoka katika diwani ya Wasakatonge: Katika hatua hii mtafiti alianza kusoma diwani teule kwa lengo la kukusanya data. Hivyo, kila alipokuwa akisoma na kubaini neno, mshororo au ubeti unahu su itikadi fulani alidondo sehemu hiyo katika shajara chini ya mada ya itikadi husika.

Hatua ya Nne: Kurudia tena kudondo data. Hatua hii ilihuisha mambo yale yale ambayo yamefanyika katika hatua ya tatu.

Hatua ya Tano: Kuunganisha data ambazo zinafanana na kuondoa zile ambazo hazitakiwi. Katika hatua hii mtafiti alipitia data zote katika shajara na kuunganisha zile ambazo zinafanana kwa kuziweka katika lengo mahususi husika la utafiti. Pia, data ambazo zilionekana kuwa hazihitajiki katika utafiti ziliondolewa na kubakiza zile zinazohitajika tu.

KIAMBATANISHO NAMBA 2: MUONGOZO WA UCHAMBUZI WA DATA
 Uchambuzi wa data ni kipengele muhimu katika kufanikisha kazi nzima ya utafiti kukamilika. Katika utafiti huu, uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Kutaja tu kwamba mkabala wa kimaelezo ndiyo uliyotumika katika kukusanya data haitoshi ni lazima kuwepo na muongozo maalumu ambao umefuatwa. Muongozo huo ndiyo huu katika hatua zifuatazo:

Hatua ya Kwanza: Kuwasilisha data. Katika hatua hii mtafiti aliwasilisha data ambazo ni madondoo kutoka katika diwani teule kulingana na mada inayohusika katika lengo mahususi la utafiti. Dondoo limewasilishwa kwa maelezo.

Hatua ya Pili: Kutoa ufanuzi wa dondo. Katika sehemu hii mtafiti alichambua data iliyowasilishwa kwa dondo na kuipatia ufanuzi ambao unakidhi mahitaji ya lengo mahususi husika la utafiti.

Hatua ya Tatu: Kuingiza nadharia katika uchambuzi wa data. Katika hautua hii mtafiti aliingiza mawazo ya nadharia katika uchambuzi wa data za utafiti.